Jumatano Septemba 16, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580340

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Mgombea wa ubunge Salim Turky afariki dunia ghafla

UKURASA 17


Kwa sheria hizi mlungula unapitaje uchaguzi mkuu? (2)

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

Oktoba 28 mwananchi unaachaje kupiga kura?

Kwa ilani hizi Tanzania isiyo na magonjwa inawezekana

■ Zahanati moja kwa watu 1,000...ACT

■ Kutibu wagonjwa KITEHEMA ...SAU

UKURASA 11

MAHOJIANO MAALUM

# Bashiru atoa sababu kuzima mzozo wa Kigwangalla na Mo

UKURASA 4



Mgombea urais kupitia tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, akihutubia maelfu ya wananchi wa Wilaya ya Muleba, mkoani Kagera jana. **PICHA: IKULU**

## JPM AAHIDI KUTATUA KERO ZAO LA KAHAWA

**AMGOMEA** Tibaijuka kustaafu siasa, Lissu aliamsha Njombe, Membe ataja kinachomkwamisha... *Endelea Ukurasa 2*



Mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akihutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu, katika viwanja vya National Housing mjini Njombe jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## MMILIKI WA SHULE ILIYOUNGUA AKAMATWA, IGP AHOJI

UKURASA 5

**MICHEZO** ZLATKO: GARI LIMEWAKA YANGA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

Fursa kwa Wagombea! 2020

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

VOTE

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz

# Lissu azigeukia hifadhi za taifa

**Na Romana Mallya**

MGOMBEA urais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amesema akipewa ridhaa ya kuongoza nchi, ataweka utaratibu mpya wa hifadhi za taifa ili uwapo wake uwe unapewa baraka na wananchi.

Lissu aliyasema hayo jana wakati akihutubia wananchi waliojitokeza kwenye mkutano wake wa kampeni mkoani Mbeya, akisisitiza kuwa ni lazima wananchi wakubali kwanza kuwa na hifadhi eneo husika.

Alisema sheria za kimataifa kuhusu masuala ya uhifadhi zinataka kuwe na ridhaa ya wananchi kuhusu miradi wanayopelekewa na serikali inayoathiri maslahi yao.

"Nani atakayeathiriwa na hiyo mipaka, atalipwaje fidia, akiondolewa atapelekwa wapi? Baada ya hayo yote ndipo waamue wanataka au hawataki, wakisema hawataki, mwisho wa habari," alisema.

Lissu alisema iwe katika kujenga barabara, kupanua shule, kujenga hifadhi, uamuzi unaothiri haki za watu, lazima wananchi watoe ridhaa yao baada ya kupata taarifa zote za mradi husika.

"Tutaitoa kwenye sheria za kimataifa na kuiweka kwenye katiba yetu, ukweli ni kwamba Jaji Joseph Warioba alituasia sana, mapendekezo mengi yapo kwenye mapendekezo ya tume ya Jaji Warioba.

"Wanafikiri maendeleo ni yale yanayotumia nguvu, sisi maendeleo ambayo Mwalimu Julius Nyerere aliandika kwenye kitabu chake ni yale ambayo hayatumii nguvu, ndiyo maana tunazungumza uhuru, haki na maendeleo ya watu.

"Tuna hifadhi za taifa zaidi ya 20, maana yake ni nini? Ukitengeneza hifadhi ya taifa unafukuza watu kwenye maendeleo, ukienda kwenye maeneo yote yenye hifadhi ya taifa ni vita na wenyeji," alisema.

Lissu pia aliahidi kuweka mfumo mpya wa kodi ili kile alichokiita mvutano kati ya Mamlaka ya Mapato (TRA) na wafanyabiashara ukome.

"Kufilisi watu na kuwabambika kodi kubwa tutayamaliza, tutaleta mfumo wa haki ya mlipakodi, kabla ya kukuambia chochote lazima akwambie una haki gani, kama anakudai, lazima aweke utaratibu wa kulipa ili usiue biashara yako kwa sababu ikifa, wanaoathirika ni wengi," alisema.

Lissu pia alitumia fursa hiyo kuzungumzia msaada wa kukodiwa ndege kwenda Nairobi kutibiwa, aliopewa na aliyekuwa Mbunge wa Mpendae, Salim Turky, ambaye alifariki dunia usiku wa jana.

# JPM aahidi kutatua shida zao la kahawa

**Na Gwamaka Alipipi,**
MULEBA

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amewasili mkoani Kagera na kutoa ahadi ya kutatua matatizo yanayolikabili zao la kahawa, ili wananchi wanufaike nalo.

Vilevile, amewataka wananchi wa mkoa huo na Watanzania kusimama katika umoja na mshikamano, ili kufanikisha kuleta maendeleo.

Alitoa kauli hiyo jana wilayani Muleba alipozungumza na wananchi waliojitokeza barabarani kumpokea akitokea wilayani Chato mkoani Geita.

Dk. Magufuli pia aliwaomba wananchi kutochagua watu wasioaminika na watakaokuja kutawala kwa matakwa ya watu wengine, badala yake wachague watu wenye uwezo wa kuongoza nchi kwa kujali maslahi ya wanyonge.

"Ninajua hapa kuna changamoto za zao la kahawa, hili nalo tunalibeba na tumeshaanza kulishughulikia, ndiyo maana wiki mbili zilizopita nilimpigia Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na wa Kilimo nao wakawatuma makatibu wakuu kuja huku kutatua changamoto za zao la kahawa.

"Tunataka tumalize matatizo ya kahawa na ninataka tuyamalize moja kwa moja maana hatuwezi kufanya miradi mikubwa halafu tushindwe kushughulikia zao la kahawa. Hapa Muleba mtuamini maana tumejipanga kufanya makubwa," aliahidi.

Kuhusu miradi iliyofanyika wilayani Muleba, Dk. Magufuli alisema kuwa Sh. bilioni 65.32 zimetumika kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Akiwa katika eneo la Kemondo, Dk. Magufuli alisema Kemondo ndiyo bandari iliyoachwa na Mwalimu Julius Nyerere na imeleta utajiri kwa watu wengi wa eneo hilo.

Alisema ni miaka 20 imepita tangu meli ya MV. Bukoba ilipozama katika Ziwa Victoria na kupoteza maisha ya watu wengi, hakujawahi kuletwa meli nyingine tangu kutokea kwa ajali hiyo, hali iliyosababisha wananchi wengi kupata tabu ya usafiri.

Alisema katika kuhakikisha usafiri wa majini unaboreshwa katika Ziwa Victoria, serikali ilikarabati meli tano pamoja na kununua meli kubwa yenye uwezo wa kuchukua abiria 1,200 na kubeba mizigo tani 400.

**AMGOMEA TIBAIJUKA**

Katika hatua nyingine, Dk. Magufuli 'aliugomea' uamuzi wa kustaafu siasa uliochukuliwa na aliyekuwa Mbunge wa Muleba Kusini (CCM), Profesa Anna Tibaijuka.

Alisema Profesa Tibaijuka bado ana uwezo wa kufanya kazi mbalimbali serikalini.

Julai mwaka jana, Profesa Tibaijuka alitangaza kujiweka kando katika masuala ya kisiasa na kueleza kuwa hatogombea tena ubunge katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Profesa Tibaijuka alinukuliwa na vyombo vya habari akitaja sababu ya kung'atuka katika ulingo wa siasa kwamba yeye ni kizazi cha Mwalimu Julius Nyerere ambaye aliwafundisha kung'atuka.

"Mimi mwaka 2020 ninastaafu, ninang'atuka kwa sababu sisi ni kizazi cha Mwalimu Nyerere na katika vitu alivyotufundisha ni kung'atuka." Alinukuliwa Profesa Tibaijuka.

Jana, Rais Magufuli akiwa mkoani hapa alisema kuwa kwake bado hajastaafu masuala ya kisiasa.

"Profesa Tibaijuka ameniambia hapa mdogo wangu nimestaafu, mimi ninakwambia Profesa haujastaafu, hatuwezi tukamwacha akakaa tu hapa wakati kuna maeneo mengi ya kufanya kazi," alisema.

Rais Magufuli alisema Profesa Tibaijuka ni dada yake na kwamba alipokuwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Mbunge wa Chato, mume wake (Profesa Tibaijuka), alikuwa Balozi Sweden.

"Mama Tibaijuka amesema amestaafu siasa, lakini kwangu mimi hajastaafu, hivyo ni faida ya kuwa na watu sehemu fulani ambao wanaweza kuisaidia serikali. Mimi ninamwambia kuwa profesa hujastaafu, hatuwezi kumwacha wakati kuna maeneo mengi anaweza kufanya kazi," alisisitiza.



Mafundi wa kampuni ya CCECC, wakiendelea na ujenzi wa barabara za juu za mpishano katika makutano ya barabara za Morogoro, Sam Nujoma na Nelson Mandela, eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Membe ataja kilichomkwamisha

**Na Enock Charles**

MGOMBEA urais kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Bernard Membe, amebainisha kilichomkwamisha kuendelea na kampeni zake zilizozinduliwa mwanzoni mwa mwezi huu.

Amesema ukosefu wa fedha, mapingamizi waliyokuwa wamewekewa wagombea wao wa ubunge na udiwani na uhitaji wa kujua hali ya afya yake ndiyo mambo matatu yaliyomlazimisha kusitisha kwa muda kampeni hizo.

Akizungumza mara tu baada ya kutua kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam jana, Membe pia aliweka wazi kuwa ni kawaida yake kwenda Dubai mara nne kwa mwaka kwa ajili ya kuchunguza hali ya afya yake.

Waziri huyo wa zamani wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, alisema anatarajia kuendelea na kampeni zake za urais Septemba 17 hadi Oktoba 26, mwaka huu bila kusimama tena kwa kuwa vikwazo vilivyokuwapo, vimetatuliwa.

Alibainisha kuwa ACT-Wazalendo inatarajia kutumia Sh. bilioni 18.2 katika kampeni hizo, Sh. bilioni 14 zikitarajiwa kutumiwa na wagombea wabunge na Sh. bilioni nne kwa mgombea urais.

"Mbio za urais ni sawa na mbio za marathon, unaweza ukakimbia ukaangalia nyuma ukacheka watu, lakini yule anayemaliza ndiye anayeshinda," Membe alisema.

"Sasa lipi bora, uchelewe ili unapoanza unakung'uta mpaka Oktoba 28 au uchomoke uanze sasa halafu ukwame baada ya wiki tatu, unabaki unakula mihogo?" Membe alihoji.

Alisema kuwa katika mbio hizo ni muhimu kujipanga vyema kimkakati, kifedha na kuwa na timu nzuri, jambo ambalo alikuwa akilifanyia kazi kabla ya kuendelea tena na kampeni zake katika mikoa mingine baada ya kuwa ameshafanya uzinduzi mkoani Lindi.

Kuhusu ushirikiano wa chama hicho na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kama ambavyo imekuwa ikipendekezwa na pande zote mbili, Membe alisema kamati za siasa za vyama hivyo zinaendelea kushauriana.

Membe alidai kuwa vyama vya upinzani vipo katika hali ngumu kifedha kuendesha kampeni zake, akitoa wito kwa wafanyabiashara nchini kutoa fedha kwa pande zote bila kuiogopa serikali.

Mgombea urais huyo pia alivishauri vyama vya siasa kutokuona aibu kuomba fedha mradi havivunji sheria huku akisisitiza kuwa asingeendelea na kampeni za urais ilhali idadi kubwa ya wagombea wao wa ubunge na udiwani walikuwa wamewekewa mapingamizi.

# Majaliwa awataka wananchi kutafakari kiongozi sahihi

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wananchi watafakari ni aina gani ya kiongozi wanamtaka aiongoze nchi.

Majaliwa alitoa wito huo jana wakati akizungumza na wananchi waliohudhuria mkutano wa kuwanadi wagombea wa CCM uliofanyika kwenye viwanja vya CCM, Kata ya Ilongero, wilayani Singida.

"Uongozi wa nchi si jambo la mchezo, si jambo la kujaribiwa wala haliendi kwa upepo na ushabiki. Ni lazima mkae na kutafakari ni nani anafaa kuongoza nchi hii," alisema na kuongeza: "Tukae tuangalie tulipo na tunakotaka kwenda. Tujiulize je, ni nani anaweza kutupeleka huko?"

Aliwataka wakazi hao wajihadhari na wagombea ambao wanatumia majukwaa kuanza kuwatukana wenzao.

"Huu siyo wakati wa kutukanana bali ni wakati wa kuelezea sera na mambo gani atawafanyia," alisisitiza.

Majaliwa alitumia fursa hiyo kuwaomba wakazi hao wamchague Rais John Magufuli, ili aongoze tena kwa miaka mitano na kumalizia kazi zilizopangwa na CCM kwenye ilani yake.

"Nawaomba wana-Ilongero, wana-Singida Kaskazini na wana-Singida wote ikifika Oktoba 28, mchagueni Dk. Magufuli. Sababu za kumwombea kura ni nyingi hasa kutokana na kazi kubwa aliyoifanya kwa nchi hii. Wote mmeona na kusikia yaliyofanyika kwenye maeneo yenu."

"Yeye ni mzuri wa kutabiri na kuyapangilia na kuyafuatilia. Yeye ni mzuri wa kutambua kero za wananchi wake na kuzitatua. Amejipambanua sana na kuwasihi wasaidizi wake wazingatie kuwatumikia Watanzania. Sote tumeona maendeleo yaliyopatikana ndani ya miaka mitano hayajapata kutokea," alisema.

Pia alitumia fursa hiyo kuwaombea kura, mbunge mteule wa Jimbo la Singida Kaskazini, Ramadhani Ighondo, na mgombea udiwani wa kata ya Ilongero, Issa Mwiru.

Wakati huo huo, Majaliwa alimpokea aliyekuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Singida, Frank Akunay ambaye ameamua kuhamia CCM.

Akunay amehamia CCM akiambatana na mkewe, Betina Ibrahim pamoja na mdogo wake, Daniel Akunay.

"Nimeamua kurudi nyumbani na nitachanja mbuga kuhakikisha CCM inashinda sababu mimi ni mtu wa 'field'. Hapa Singida Kaskazini tuna vijiji 84, vitongoji 435 na kata 21. Ninavijua vyote. Nakuhakikishia tutashinda kwa asilimia 98 sababu sijarudi kwa bahati mbaya," alisisitiza.

"Tuna uhakika wa kupata ubunge kwani anayegombea hatusumbui kabisa. Kwa madiwani, tumebakiza kata 19 kwani wawili walishapita bila kupingwa."



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akimsikiliza, aliyekua Mwenyekiti wa CHADEMA, Singida Kaskazini, Frank Petro (kulia), baada ya kuhamia rasmi CCM, katika mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu, uliyofanyika kwenye viwanja vya Ilongero, mkoani Singida, jana. **PICHA: OWM**

# Nchi 15 kuleta waangalizi wa uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeziruhusu nchi 15 kupitia balozi zao nchini zimeruhusiwa kuleta waangalizi wa kimataifa katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, 2020.

Hayo yamebainishwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi na kwamba

hatua hiyo imechukuliwa baada ya balozi hizo kuwasilisha maombi na kufuata taratibu.

Prof. Kabudi aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU), Balozi Manfred Fanti na kuongeza kuwa uchaguzi wa mwaka huu kwa mara ya kwanza umekuwa tofauti na miaka iliyopita, kwa kuwa unafanyika kwa kugharamiwa na fedha za ndani badala ya wahisani jambo ambalo baadhi ya watu walianza kuhofia kutokuwapo kwa waangalizi wa kimataifa.

"Huu ni uchaguzi mkuu ambao kwa mara ya kwanza kwa asilimia 100 tunaugharamia sisi wenyewe kama Serikali ya Tanzania, utaratibu wa uchaguzi chini ya sheria ya uchaguzi na chini ya utaratibu wa kimataifa huwa tunakuwa na waangalizi wa uchaguzi na mwaka huu nchi hizo 15 kupitia balozi zao zimepata kibali baada ya kufuata taratibu za kuomba kuleta waangalizi wa uchaguzi mkuu," alisema Prof. Kabudi.

Mbali na huyo wa EU, pia Prof. Kabudi alikutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Italia nchini, Balozi Roberto Mengoni na baadaye Balozi wa Poland, Balozi Krzysztof Buzalski ambapo amewakabidhi vitabu vya sheria ya uchaguzi na kanuni za uchaguzi na miongozo mbalimbali inayohusu masuala ya uchaguzi ili kuwapa fursa ya kufahamu namna uchaguzi unavyoendeshwa nchini hususani baada ya uwapo wa malalamiko kutoka kwa baadhi ya vyama vya upinzani juu ya kuenguliwa kwa wagombea wao.

Kwa upande wake Balozi Fanti alisema Nchi za Umoja huo zimekuwa zikifuatilia kwa karibu mchakato wa kampeni za uchaguzi mkuu zinavyoendelea nchini ambapo mpaka sasa wanaridhishwa na kampeni zinavyofanyika kwa uhuru na amani na sasa wanajiandaa na zoezi la uangalizi wa uchaguzi huo.

Balozi wa Italia nchini Roberto Mengoni, alisema amevutiwa na namna vyombo vya habari vimekuwa vikitoa nafasi kwa wagombea wote kwa uhuru na bila ya ubaguzi na kupongeza namna Watanzania wanavyojitokeza kwa wingi kusikiliza sera za wagombea mbali na tishio la corona, na kwamba ana imani kuwa kiongozi atakayechaguliwa atakuwa ametokana na utashi wa wananchi.

Mbali na masuala ya uchaguzi mkuu, Waziri Kabudi na Mabalozi hao walijadili pia masuala ya kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia, maendeleo ya kiuchumi, biashara na uwekezaji katika sekta mbalimbali ikiwamo elimu, afya, maji na miundombinu.

**BODI YA MICHEZO YA KUBAHATISHA TANZANIA**

GAMING BOARD OF TANZANIA

Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT) inapenda kutoa taarifa kwa waendeshaji wa mchezo wa Pool Table kuwa, uendeshaji wa mchezo wa Pool Table unasajiliwa na kuratibiwa na GBT ambayo ni taasisi ya Serikali yenye jukumu la kusimamia uendeshaji wa michezo yote ya kubahatisha hapa nchini.

Kwa mujibu wa Kifungu Namba 52 cha Sheria ya Michezo ya Kubahatisha ya mwaka 2003, Pool Table zote zinatakiwa kusajiliwa na GBT na kupatiwa leseni. Hivyo waendeshaji wote wanatakiwa kufanya usajili wa Pool Table zao na kupatiwa leseni husika itakayowawezesha kuendesha michezo hiyo kihalali na kwa kufuata sheria.

Ikimbukwe kuwa kuendesha mchezo wa pool table bila ya usajili na leseni halali ni kosa kisheria. GBT inawatahadharisha waendeshaji wote wa mchezo wa pool table nchini kuwa, endapo watabainika kukiuka agizo hili hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.
Aidha, GBT imeazimia kufanya msako nchi nzima kubaini watakao kaidi agizo hili ili Sheria ichukue mkondo wake.

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania**
**Ghorofa ya 27, PSSSF Towers**
**Mtaa wa Mission/Sokoine Drive**
**S. L. P. 1717**
**Dar Es Salaam. TANZANIA.**
**Simu: +255222124703/4 au 0800 110051**
**Barua Pepe: info@gamingboard.go.tz**

215899302

# Bashiru aanika sababu kuuingilia mvutano Kigwangalla, Mo Dewji

## ■Awaonya wagombea ubunge wa CCM

Na Thobias Mwanakatwe, DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amebainisha sababu za chama hicho kuingilia kati mvutano ulioibuka hivi karibuni kati ya Dk. Hamisi Kigwangalla na Mohamed Dewji, maarufu Mo.

Wiki mbili zilizopita, kuliibuka majibizano kupitia mtandao wa kijamii wa Twitter kati ya Mo Dewji na Waziri huyo wa Maliasili na Utalii kutokana na kile ambacho Kigwandalla alidai mfanyabiashara huyo maarufu kutotekeleza matakwa ya mkataba wa uwekezaji katika Klabu ya Simba ya jijini Dar es Salaam.

Kufuatia hali hiyo, Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru alizungumza na waandishi wa habari akimtaka Dk. Kigwangalla kuacha mara moja kujibizana na mfanyabiashara huyo na kujikita katika kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Dk. Kigwangalla anawania tena ubunge wa Nzega Vijijini na ni miongoni mwa wagombea ubunge 18 wa CCM ambao wametangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kupitia bila kupingwa.

Katika mahojiano yaliyorushwa na kituo cha runinga cha ITV kupitia cha 'Dakika 45' usiku wa kuamkia jana, Dk. Bashiru alisema aliamua kuingia mvutano huo baada ya kubaini hatari ya kukikosesha chama kura.

Aliwaonya wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi kupitia chama hicho, hususani waliopita bila kupingwa katika nafasi ya udiwani na ubunge, kudhani kuwa wapo huru kufanya mambo yao binafsi.

"Mgombea wa CCM katika kipindi cha kampeni za uchaguzi mkuu hana maisha binafsi, ndiyo maana ninataka kujua hata alikolala, chakula anachokula, ninataka kujua ratiba yake ya kila siku, ninataka kujua amesema nini, amekutana na nani, amepanga nini ili tupate ushindi. Kwa hiyo, hawa ni wagombea chini ya CCM," alisema.

Dk. Bashiru alisema wagombea wa CCM lazima watambue kuwa wanaosimamia maisha ya siasa kipindi hiki ni Kamati Kuu (CC) ya chama ambayo maagizo yake ni lazima yatekelezwe.

Alisema baadhi ya wagombea waliopita bila kupingwa walidhani wako huru bila kutambua kuwa wanatakiwa kushiriki kampeni kwenye maeneo yao kuwaombea kura wagombea wenzao ambao hawajapita bila kupingwa.

"Tunawakumbusha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hajapita bila kupingwa, Rais wa Zanzibar hajapita bila kupingwa na hatuwezi kuwa na ushindi wenye thamani na maana kama hatujashinda ngazi ya urais.

"Kama mtu ana muda wa kuandika kwenye mitandao ya kijamii masuala ya mpira na anapata wafuasi na kule kwenye ubishani kunaweza kukasababisha kutunyima kura, ni lazima tumkumbushe wajibu wake," alisema.

Alisema wagombea hao wanapaswa wazitumie ratiba walizokuwanazo awali kwa ajili ya kampeni kufafanua vizuri kwa wananchi mambo yaliyofanywa na serikali, yaliyoahidiwa ndani ya miaka mitano na kuwaombea kura wagombea ambao hawakubahatika kupita bila kupingwa.

Kuhusu agizo la chama kwa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) kujibu mapigo kwa wapinzani, Dk. Bashiru alifafanua kuwa wamefanya hivyo kwa sababu kampeni za mwaka huu zina viashiria visivyo vya kawaida.

Alisema kuibuka kwa viashiria hivyo anafiki kumetokana na baadhi ya wanasiasa kutokujiandaa kufanya kampeni kwa hoja badala yake wanalenga kuichafua CCM na mlengwa mkuu ni mgombea wa urais wa chama hicho. "Tulichukua msimamo wa kuwapuuza na hayo yalikuwa ni maagizo ya Mwenyekiti (Dk. John Magufuli), wakati mwingine kinachofanywa ni kebehi, matusi na uchochezi, jambo ambalo likiachwa linaweza kuwa na madhara. Sisi tuna utamaduni wa kuvumiliana kisiasa, kusema ukweli," alisema.

Dk. Bashiru alisema siyo kwamba CCM haitaki kukosolewa, bali inataka ukosoaji uzingatie hoja za kweli kwa kuwa lengo la vyama vyote ni kujenga taifa moja, kulinda uhuru na kuimarisha utaifa.

"Ikitokea wanasiasa ambao wanataka kututoa katika misingi hiyo ambayo kwa kweli ni utamaduni mpya, CCM haiwezi kunyamaza na kwa sababu tuko wengi, nikianza kuwafungulia hao watu wajibu watapoteana," alitamba.

Alipoulizwa kuhusu dosari ya wagombea kupita bila kupingwa kwa nchi ya kidemokrasia kama Tanzania, Dk. Bashiru alisema uchaguzi nchini unasimamiwa kwa mujibu wa sheria na kila penye haki pana wajibu.

"Vipo vigezo vya kuwa mgombea udiwani, ubunge na mgombea urais. Usipokidhi vigezo hivyo, maana yake unamwachia aliyekidhi vigezo," alisema.

Dk. Bashiru aliongeza kuwa wanaolalamika wakidhani kuna rafu inachezwa, inabidi wawe na kumbukumbu kwamba uchaguzi wa mwaka huu siyo wa kwanza kufanyika ndani ya mfumo wa vyama vingi, akikumbusha kuwa ulikuwapo tangu mwaka 1995 na wagombea walikuwa wakipita bila kupingwa, hivyo siyo jambo jipya.

"Sasa kama chama hakina uwezo wa kuwasimamia wagombea wake na wagombea wengine hawana ufahamu na chama hakina mtandao wa kutosha, hakina uzoefu wa kutosha, hatimaye wagombea wanakosa msaada na maelekezo ndicho kinachokuja kutokea, wasitafute lawama wakishindwa," alisema.

Mtendaji huyo wa CCM alisema hawahusiki na uzembe na udhaifu wa mgombea yeyote au chama chochote kwa kuwa kazi ya CCM ni kuhakikisha kila anayeingia uwanjani, inamshinda na kwamba mwaka huu watarajie kipigo cha mwaka ili kutoa fundisho kwamba suala la uongozi siyo la majaribio.

"Tunavyozungumza hapa, kuna mgombea mmoja wa urais yuko Dubai na kule kuna wanachama wetu wanamwona na kujiuliza 'huyu kakimbia uchaguzi au vipi?'

"Mgombea wetu yuko Geita, akitoka huko anakwenda Kagera, Kigoma na Tabora... sasa huyo aliyekwenda Dubai katikati ya kampeni, akisema nimeonewa akaanza kulalamika wapigakura watampima," alisema.

Kuhusu madai kwamba CCM inawatumia wasanii na kuwabeba watu kwenye malori kuwapeleka kwenye mikutano yake ya kampeni, Dk. Bashiru alisema hakuna kitu kama hicho, akifafanua kuwa wasanii ni Watanzania, siyo watumwa ni watu wazima na hawawezi kulazimishwa.

"Unambebaje mtu kama Diamond, Alikiba, Harmonize, Zuchu, Mrisho Mpoto na wengine wengi, tuwabebe kwanini? Ni kwamba wamevutiwa na kazi nzuri ya kujenga taifa iliyofanywa na serikali ya CCM," alisema.

Aliongeza kuwa wasanii hao hawalipwi na chama bali wanajigharamia wenyewe.

Kuhusu suala la serikali kumiliki ndege badala ya biashara hiyo kufanywa na watu binafsi, Dk. Bashiru alihoji kama nchi ina Mtanzania anayeweza kumiliki ndege.

Alisema kwa kuwa nchi haina kampuni binafsi ya kumiliki ndege, serikali imeamua kujidunduliza kwa pesa za nchi na kununua ndege zake.

"Kuna njia mbili za kumiliki ndege, ama kwa mtaji wako wa mtu mmoja au mtaji kwa pamoja, hizi ni ndege za Watanzania, ni kampuni za Watanzania, suala la wamezimiliki kwa mfumo gani, ni jambo lingine," alisema Dk. Bashiru.



Dk. Bashiru Ally



Mohammed Dewji 'MO'.



Hamisi Kigwangala

## HABARI KITAIFA

# Taasisi za mikopo kwa vitambulisho vya NIDA zaonywa

**Na Frank Maxmillian,** TUDARCo

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imetoa onyo kali kwa taasisi zinazochukua vitambulisho vya wananchi kwa ajili ya kutoa mkopo.

Imezitaka taasisi hizo kuacha mara moja na kurejesha vitambulisho hivyo vinginevyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na NIDA jana, baadhi ya watu, vikundi vya watu na taasisi binafsi nchini kutoa mikopo zinawalazimisha wakopaji kupeleka kitambulisho cha taifa na kukiacha kwa mkopeshaji.

"NIDA inawataka waliochukua vitambulisho hivyo kuvirejesha au kuvipeleka katika ofisi yoyote ya NIDA au kituo chochote cha polisi kilichopo jirani haraka iwezekanavyo," lilisema sehemu ya tangazo hilo.

Akizungumza na Nipashe, Msemaji wa NIDA, Geofrey Tengeneza, alisema hivi karibuni walipokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa vitambulisho vyao vinashikiliwa na taasisi hizo hadi watakapolipa madeni yao.

"Hairuhusiwi kisheria kuchukua kitambulisho cha mtu na kukaa nacho, hata benki kama unataka mkopo au huduma inayohitaji kitambulisho watatoa nakala na kukurudishia, sasa iweje hawa wanachukua vitambulisho na kukaa navyo kama dhamana ya mkopo, hili halikubaliki na ndiyo maana tumewaonya na kuwataka kuacha mara moja," alisema.

Alisema kama taasisi hizi zinaendesha biashara ni vyema zikafuata taratibu za kisheria na uchunguzi unaendelea kwa ambao watakaidi watakamatwa na kufikishwa mahakamani.



Mgombea urais kupitia Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, akihutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu katika uwanja wa shule ya Medeli, jijini Dodoma juzi jioni. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# IGP ahoji mamlaka kuruhusu shule yenye majengo mabovu

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI polisi wanamshikilia mmiliki wa Shule ya Msingi ya Kiislamu Byamungu, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Siro, amehoji mamlaka ziliruhusu vipi shule hiyo kufunguliwa wakati majengo yake yakiwa chini ya kiwango na kiusalama.

Ajali hiyo ya moto ilitokea usiku wa kuamkia juzi katika shule hiyo iliyoko wilayani Kyerwa mkoani Kagera na kusababisha vifo vya wanafunzi 10 na majeruhi sita. Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kutembelea eneo la tukio jana, IGP Sirro alisema tayari mmiliki wa shule hiyo anashikiliwa na kwamba wale wote waliohusika na ajali hiyo watawajibishwa.

"Ukiliona jengo lenyewe sijui kama wakaguzi, ofisa elimu walikuwa wanajua watoto walikuwa wanalala katika jengo hili. Ukiangalia mfumo wa umeme ndani ya nyumba uliofanywa ni wa kienyeji sana," alisema Sirro. Alisema jengo hilo linaonekana halikuwa madhubuti na utaratibu wa uwekaji mfumo wa umeme ulipitishwa kwa chini.

"Inaonekana halikuwa na mpango mzuri wa kuingiza umeme kwenye jengo na matofali ni ya kuchoma ya udongo ukiyaangalia yapo dhaifu sana, yamesababisha vifo vya vijana wetu.

"Vijana 10 wamefariki (dunia) katika tukio hili na wanne hali zao ni mbaya. Tumekwenda kuwaangalia hospitalini, tunafanya uchunguzi wa tukio," alisema.

IGP Sirro alisema mpaka sasa Jeshi la Polisi halijajua chanzo cha ajali hiyo ingawa kwa haraka inaonekana jengo hilo halikuwa madhubuti.

"Mwenye shule ameshakamatwa, lakini pia nimeagiza atafutwe ofisa elimu na wakaguzi wote waliokuwa wanakuja kukagua hii shule. Walikuwa wanaona watoto wanakaa wapi? Jengo lilikuwa imara?" Alihoji.

"Ni lazima hapa tuwe wakali kwa sababu tayari maisha ya watu yamekwisha ondoka. Kingine tunajaribu kutafuta vyanzo vingine, inawezekana jengo halikuwa madhubuti, lakini inawezekana kuna adui wa nje amechukua huo mwanya kufanya uhalifu," alisema.

IGP Sirro alisema wako makini na suala hilo na kwamba wapelelezi watakwenda eneo la tukio na watapata majibu, huku akiwataka wana Kyerwa kutoa ushirikiano wa taarifa zozote za ajali hiyo.

"Bahati nzuri mkuu wa wilaya ana msaada sana atatusaidia kuzipata, tukipata taarifa kamili niwahakikishie tutawashughulikia kweli kweli, hatuna mchezo, hatuna mchezo kwa mtu mwenye uzembe wake au kwa nia ovu anasababisha vifo vya Watanzania," alisema.

IGP Sirro alisema aliwahi kueleza kuwa damu ya Mtanzania haiendi bure, lazima aliyesababisha ashughulikie kwa mujibu wa taratibu.

Muuguzi kiongozi wodi ya watoto katika Hospitali Teule ya Nyakahang, wilayani Karagwe, Theophilda Ndibalema, alisema majeruhi wa moto huo wamehamishiwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda, Bugando iliyoko jijini Mwanza.

Ndibalema aliwataja waliohamishiwa Bugando kuwa ni Lukumani Said Ramadhan (7), Imani Majaliwa Hatuna (12), Sshraf Mohamed (7) na Juma Seif Juma (12).

Pia alitaja majeruhi wawili waliobaki katika Hospitali ya Nyakahanga kuwa Avitus Sperius (8) na Swabrudin Swaibu (11).

Sperius Bernard ambaye ni mzazi wa mtoto Avitus alisema alipata taarifa za tukio hilo na kufika shuleni saa tisa usiku alikuta tayari mtoto wake amepelekwa Hospitali ya Nyakahanga.

**Imeandaliwa na Romana Mallya (Dar) na Lilian Lugakingira (Kyerwa).**


## BANI INVESTMENT LIMITED

### DEBT COLLECTORS/ AUCTIONEERS

### NOTISI YA SIKU 14/TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **BENKI YA NBC MAKAO MAKUU** tunatoa notisi ya siku 14 na tangazola mnada wa hadhara wa mali zilizoorodheshwa hapo chini ambazo ziliwekwa kama dhamana ya mkopo. Hivyo basi utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili, Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada.Mnada utafanyika mahali zilipo mali hizi, kama ilivyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo:-

| JINA LA AKAUNTI | MMILIKI | MALI ZILIZOWEKWA DHAMANA | MAHALI |
|---|---|---|---|
| Aloyce W Lupondo | ALOYCE LUPONDO | Nyumba yenye CT NO 8107 MBYLR PLOT NO 252 BLOCK EE LAND OFFICE NO 174015 | Kalumbulu-Kyela |
| Godwill A Kidulile | GODWILL ALLEN KIDULILE | OFFER OVER FARM NO. 92 | Kibao Mtwango-Mufindi |
| JUMA ABDALLAH SADICK | JUMA ABDALLAH SADICK | PLOT NO "11" | Tuangoma-Temeke |
| Zuberi S. Zuberi | ZUBERI SAID NYARI. | Nyumba yenye CT NO.10014-LR MOSHI, L.O.NO.136103, PLOT NO.127 BLOCK 'N' SECTION IV | Majengo-Moshi |
| JOSEPH ISSAYA KILIMBE | JOSEPH ISSAYA KILIMBE | Nyumba yenye CT NO.15995-DLR, L.O. NO.96253/10416, PLOT NO.10, BLOCK 'M' | Chang'ombe-Dodoma |
| ROBERT CHARLES KISWAGA | ROBERT CHARLES KISWAGA | Nyumba yenye CT NO.11949 PLOT NO 30 BLOCK C | Ubaruku |
| Agape P Nkya | AGAPE PIUS NKYA | Nyumba yenye CT NO. 20185-LR MWANZA L.O NO. 301428, PLOT NO. 295, BLOCK 'L', | Nyakato-Mwanza |
| Julius Mafuru Mhoji | JULIUS MAFURU | Nyumba yenye CT NO. 21168-LR MWANZA, L.O. NO. 301722, PLOT NO.762, BLOCK 'HH' | Nyakato-Mwanza |
| John N Magina | JOHN NDALAHWA MAGINA | Nyumba yenye CT NO. 21505, L.O.NO.181753,PLOT NO. 827,BLOCK 'Q' (HD) | Nyasubi-Kahama |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mali zitauzwa "kama zilivyo " as is where is basis"
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki ni juu ya mnunuzi
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wowote isipokuwa usiku.

215902402

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na Ofisi ya:**
**Kwa maelezo zaidi wasiliana Na ofisi ya BANI INVESTMENT LTD Nkurmah Street, Lida Building, Ghorofa ya 3, Chumba No. 0313 S.L.P 71340 Dar es Salaam au kwa simu na. 0713 224578, 0622 020147,0653 640999**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Matukio ya moto shuleni yanahitaji ufumbuzi sasa

**JUZI** wanafunzi 10 wa Shule ya Msingi ya Kiislamu Byamungu, iliyoko Kata ya Kyerwa wilayani Kyerwa mkoani Kagera, waliteketea kwa moto kiasi cha miili yao kutofahamika, huku wengine sita wakijeruhiwa baadhi vibaya, kutokana na bweni walilokuwa wamelala kuungua moto ambao chanzo chake hakijajulikana.

Tukio hili ni la tano kutokea kwa shule za sekondari na msingi za kiislam nchini ikiwa ni matukio mawili kwenye shule hiyo ambayo hayakusababisha madhara yoyote.

Mengine ni kwa Shule ya sekondari ya Ilala Islamic iliyoungua mwezi Julai, mwaka huu na kusababisha vifo vya wanafunzi wawili pamoja na shule ya Mivumoni Islamic iliyopo Msikiti wa Myambani Kinondoni mkoani Dar es Salaam, ambako mali ziliteketea kwa moto.

Baada ya matukio hayo ya mfululizo kwa Jiji la Dar es Salaam, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliagiza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, kuunda kamati ya kuchunguza tukio hilo.

Aidha, baada ya kutokea tukio la shule ya Byamungu, Mkuu wa mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alitangaza kuundwa kwa kamati ya kuchunguza chanzo cha matukio ya moto kwenye shule hiyo ili kuchukua hatua zaidi.

Licha ya kamati zote kutotangaza walichobaini mbele ya umma, lakini bado yapo maswali mengi na magumu ya kujiuliza juu ya hiki kinachotokea ambacho kinaendelea kusambaa na sasa madhara yamekuwa makubwa.

Maswali haya ni je, shule hizi zinachomwa moto au zinaungua ikiwa ni majanga kama majanga mengine, je, ni matukio ya kawaida kabisa au yana ajenda nyuma ya pazia, je, ni kwanini shule zinazoungua ni za Jumuiya moja pekee? Je, kamati zimebaini nini na hatua gani zimechukuliwa ili kupeusha, Je, ni miundombinu ya muda mrefu?

Lakini kubwa tunajiuliza ni kwa namna gani ofisa elimu na wakaguzi wa elimu waliridhika na majengo hayo na kuruhusu yaendele kutumiwa na wanafunzi 74.

Ni lazima maswahi haya yajibiwe kupitia kamati zilizoundwa, na kubwa zaidi lipatikane jibu ni kwanini shule zinazoungua ni hizi na kwanini hali iko hivyo?

Matukio haya yanatoa taswira kuwa lipo tatizo la msingi sana katika miundombinu ya shule hizi, na badala ya kufanya jambo kwa zima moto wa kundana na upepo uliopo ni wakati wa kuhakikisha shule zinakaguliwa mara kwa maa na ndiyo maana kuna wakaguzi wa elimu.

Katika moja ya mahojiano, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, alisikika akishangaa jinsi miundombinu ya shule hiyo ilivyokuwa dhaifu, huku akihoji ilikuwaje wakaguzi na ofisa elimu kuruhusu shule hiyo kuwa na wanafunzi.

Maswali anayojiuliza ndiyo wanayojiuliza Watanzania kwamba shule yenye miundombinu dhaifu kiasi hicho inaruhusiwaje kuendelea kuhifadhi wanafunzi, na kama ukaguzi ungefanyika inavyotakiwa maana yake hatua zingeeshachukuliwa.

Kuna wakati ilitokea tukio la ajali ya gari kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Lucky Vincent jijini Arusha, na kusababisha vifo vya wanafunzi 32, hatua zilizochukuliwa kwa haraka ambazo kwa sasa hazisimamiwi na baadhi ya shule ni kuelekeza magari ya kupakwa rangi ya njano.

Kwa sasa baadhi ya magari yanabeba wanafunzi, lakini hayana vigezo vya kisheria vya kufanya hivyo, jambo hili likiachwa maana yake yakitokea maafa mengine ndiyo utakuja mkakati mwingine.

Tunasema suala hili la matukio ya moto kwenye hizi shule lifanyiwe uchunguzi wa kina, hatua zichukuliwe kwa uzembe wowote uliojitokeza, kuwapo na uwajibikaji kuanzia mmiliki wa shule hadi watumishi wa shule na mamlaka za serikali.

Hatuoni tija kwa kufumbia udhaifu unaosababisha matukio haya, badala yake kuanza kutafuta 'mchawi' kila majanga ya moto kwenye shule.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Buriani Turky, wapigakura Mpendae watakukumbuka



Na Christina Mwakangale

**MGOMBEA** ubunge aliyetarajia kuwania kiti cha ubunge wa jimbo la Mpendae visiwani Zanzibar, Salim Hassan Turky, amefariki dunia zikiwa zimesalia siku 42 kabla ya kufanyika uchaguzi mkuu. Wa Oktoba 28.

Kifo chake kilichotangazwa na vyombo mbalimbali vya habari vikimnukuu Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Hamphrey Polepole, akielezea masikitiko ya chama kufuatia kifo hicho cha ghafla kilichotokea juzi jioni.

Alifariki dunia katika Hospitali ya Global iliyopo mjini Zanzibar wakati akipatiwa matibabu baada ya kuugua ghafla, kwa mujibu wa taarifa za wanafamilia yake.

Kifo cha Turky maarufu kama 'Mr White' kutokana na mtindo wake wa kuvalia mavazi meupe akiwa bungeni na kwenye mikusanyiko mbalimbali kinaurejesha tena mchakato wa kutangaza nia, uteuzi na kuanza kampeni upya katika jimbo la Mpandae aliloliongoza tangu mwaka 2010.

Wapigakura wa jimbo la Mpendae pia wamepata pigo wakati hivi sasa kampeni za uchaguzi zikiwa zimeshika kasi nchi nzima kwa wagombea wa udiwani, ubunge, uwakilishi na urais kuendelea kunadi sera zao kwa wapigakura.

Mgombea huyu alikuwa maarufu kwa jina la 'Mr White' kutokana na uvaaji wake wa nguo nyeupe, alikuwa, akitetea kiti hicho baada ya kuwa mbunge kuanzia mwaka 2010 hadi mwaka huu.

Mwanasiasa Turky ni kijana katika uwanja wa siasa aliyezaliwa mwaka 1963 atakumbukwa kwa mchango wake katika sekta nyingi ukiwamo usafirishaji, uzalishaji viwandani na michezo.

Kwenye michezo alikuwa anashiriki wa hali na mali kuinua michezo visiwani Zanzibar kwa kuichangia timu ya taifa.

Katika hilo wadau wa michezo pia wanamlilia wakimkumbuka kwa kujitoa kwake kwa kuwa mwaka 2017 Salim Hassan Turky aliwahi kuzichangia fedha timu ya Zanzibar Heroes, ambayo inashiriki michuano mbalimbali ikiwamo ya Klabu Bingwa ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

> **Mchakato huo huanzia katika vyama kwa wagombea kutangazania, kuchukua fomu hadi kuteuliwa. Mchakato huo jimboni Mpendae utasimama hadi Tume ya Taifa ya Uchaguzi itakapotangaza, ratiba na taratibu nyingine za kisheria.**

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu unatarajiwa kufanyika Jumatano Oktoba 28 ambao Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imeshatangaza jumla ya majimbo ya Tanzania Bara na visiwani Zanzibar, Mpendae haitashiriki.

Katika siku za mwisho za maisha yake kisiasa, wengi walishuhudia wiki iliyopita Septemba 12, Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akimnadi mgombea huyo Salim Turky katika uzinduzi wa kampeni za CCM zilizofanyika viwanja vya Demokrasia Kibandamaiti.

Hatua hiyo inaweza kufananishwa na kuwaaga wapiga kura wake na wananchi pia kuagana na kiongozi wao.

Kutoka na kifo cha Turky, kanuni na sheria za uchaguzi zinabainisha kuwa jimbo au kata inapoteza sifa ya kushiriki iwapo mgombea amefariki au kuhama chama.

Kutokana na taratibu hizo Mpendae inapoteza sifa hiyo, na uchaguzi katika jimbo hili utasitishwa na kusubiri mchakato mpya kama ilivyokuwa awali katika kuwapata wagombea kutoka vyama mbalimbali vinavyoshiriki.

Mchakato huo huanzia katika vyama kwa wagombea kutangazania, kuchukua fomu hadi kuteuliwa.

Mchakato huo jimboni Mpendae utasimama hadi Tume ya Taifa ya Uchaguzi itakapotangaza, ratiba na taratibu nyingine za kisheria.

Ni wazi kuwa washabiki wake wa Mpendae wamepata pigo kubwa kwa kuondokewa na kiongozi wao huyo ambaye huenda walimtegemea kuwaongoza tena kwa miaka mitano ijayo.

**Buriani Turky.**

## HABARI KITAIFA

# Mwinyi aahidi mfumo maalum wa uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema iwapo atapata ridhaa ya kuiongoza Zanzibar ataweka mfumo maalum kwa wawekezaji wanaotaka kuwekeza katika ukanda wa utalii kupewa kibali maalum, ili Wazanzibari waweze kunufaika.

Akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Kusini Unguja, wakati wa ziara yake ya kusikiliza kero za wananchi katika vijiji mbalimbali vya wilaya hiyo, alisema mfumo huo pia utakuwa maalum kwa wawekezaji hao, ili maeneo wanayonunua yanaendelezwe.

Alisema, maeneo mengi yamekuwa yakichukuliwa na wawekezaji hali ambayo inasababisha wananchi kukosa fursa za kujiajiri kupitia sekta hiyo.

"Wawekezaji tunawataka na kuwahitaji, lakini hatutaki kuona wanapewa ardhi bila ya kuuendeleza, akishindwa ananyang'anywa na kupewa mtu mwingine iweze kuendelezwa, ili serikali na wananchi waweze kunufaika," alisema.

Alisema, utalii ni sekta muhimu katika visiwa vya Unguja na Pemba ikiwamo fukwe, maeneo ya kihistoria na hoteli, hivyo serikali itaendeleza sekta hiyo kwa kuongeza idadi ya watalii wanaoiingia nchini kutoka 500,000 na kupokea zaidi ya 850,000.

Alisema serikali atakayoiongoza itaondoa dhuluma na upendeleo hasa katika upatikanaji wa ajira serikalini, ili kila Mzanzibari mwenye sifa ya kuajiriwa apate haki yake.

Alisema, atahakikisha suala hilo analifanyia kazi kwa umakini mkubwa na anafahamu changamoto zilizopo katika sekta hiyo serikalini.

Alisisitiza kuwa, amegombea nafasi hiyo kwa dhamira ya kuwatumikia Wazanzibari ikiwamo kusikiliza matatizo ya wananchi na kuyafanyia kazi.

Dk. Mwinyi, aliwataka wananchi kumwamini, kuona kazi hiyo na kazi nyingine anazifanya kwa nguvu na maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Pia alisema serikali ya awamu ya nane itaweka kipaumbele sekta ya uvuvi, ili iweze kuwanufaisha wananchi na bado Wazanzibar hawajanufaika na sekta hiyo.

Akizungumzia changamoto ya udhalilishaji, Dk. Mwinyi aliwahakikishia wananchi atashirikiana na wanajamii, ili kuunganisha nguvu za pamoja kuondoa tatizo hilo kabisa.

Aliahidi kuviwezesha vikundi vya ushirika kwa kuongeza mfuko wa uwekezaji, ili kinamama waweze kujiwezesha kiuchumi.

# Sumaye awataka wanaCCM kuacha makundi

**Na Edna Alex,** SINGIDA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Fredrick Sumaye, amewataka wagombea wa nafasi za ubunge na udiwani kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), kuacha makundi ili kukisaidia chama kupata ushindi wa kishindo.

Sumaye aliyasema hayo jana alipokuwa akizindua kampeni za ubunge na udiwani, Jimbo la Singida Kaskazini, mkoani Singida zilizofanyika katika eneo la Kata ya Itaja. "Mlikuwa wengi kwenye mchakato huu wa kuwania nafasi hizi, lakini sasa tumeshawapata wagombea hivyo tuwaunge mkono hao, nategemea kuwaona ninyi mliokosa nafasi hizi kushiriki kwenye kampeni ili kuwaunga mkono hao wagombea," alisema Sumaye.

Alisema kutokana na maendeleo makubwa yaliyofanywa na Dk. Magufuli chini ya CCM, wananchi wanapaswa kumchagua kuendelea kuwa rais na wabunge pamoja na madiwani wa chama hicho ili kukamilisha yote ya kimaendeleo aliyotarajia kuifanyia Tanzania.

Vile vile, Sumaye alisema Mwalimu Nyerere, aliikabidhi nchi kutoka mikononi mwa wazungu hivyo Watanzania hawatakuwa tayari kuwaachia wapinzania ambao hata kuongoza wilaya hawajawi na kuhoji kama wataweza kuiongoza nchi.


TADB
Tanzania Agricultural Development Bank
"The Farmers' Bank"

## Partnering in the Operationalization of TADB's Integrated Agricultural Value Chain Financing model

215903101

**Introduction:**

Expression of Interest is requested by the Tanzania Agricultural Development Bank Limited (TADB) from interested parties to form a pool of institutional experts to partner with the bank, as project implementers/administrators to design and implement agricultural projects which follow the Integrated Agricultural Value Chain Financing Model recently adopted by the bank. The partnership entails the design and implementation of agricultural projects which brings together various actors in agricultural value chains to play different roles in the implementation of TADB financed projects with the view to create the much needed synergies necessary to create sustainable agricultural value chains.

The ideal partners will have demonstrated experience in the design and implementation of inclusive agricultural value chain projects focusing on, among others, enhancing the productivity and expanding production by small scale farmers by supporting greater access to inputs and technologies, training and extension services, financial services and facilitating guaranteed off-take by traders and agro-processors. The ideal partners will also demonstrate thorough understanding of agricultural value chains of their interest and specialization. This will include, but will not be limited to, understanding of the key players in the value chains of focus, their organization, interests, roles, influences and interactions; production and market characteristics; opportunities, incentives and disincentives along the various segments of the chains; and the institutional, legal and regulatory environment of the same.

**Projects will be designed following a collaborative approach with specific responsibilities for each partner as will be defined by framework agreements (joint MOUs) to be signed by the partners. Some of the key partners envisioned include, but not limited to;**

i. **Producer groups** (crop, livestock, fisheries and forestry); who are the target beneficiaries of supported projects;

ii. **Input and technology suppliers** including suppliers of seedling, seeds, fertilizers, agro-chemicals, farm implements, tractors and related technologies;

iii. **Off-takers and/or agro-processors;** to determine produce specification and ensure reliable off-take from producer groups.

iv. **LGAs:** to make possible the supply of reliable extension services, assist in project monitoring and enforce contracts between producer groups and off-takers/agro-processors;

v. **Research institutions:** to play the R&D role including researching and/or developing seeds and seedlings and facilitate their distribution to farmers;

vi. **Project implementers/administrators:** to play the overall project coordination role and bring together various actors (mentioned above) along the various agricultural chains and the services of various support institutions.

vii. **Project Manager:** where appropriate, a project management professional may be engaged to provide expertise in conceptualizing projects, planning, overseeing execution, management and closing as appropriate.

viii. Any other partners as specific projects may require.

**Below is a schematic depiction of the Integrated Value Chain Financing Model which will inform the design of projects to be implemented under this arrangement (for illustrative purposes only – actual project designs may differ depending on value chain specific characteristics).**




**Submission of Expression of Interest**

Interested parties must provide information indicating that they are qualified to perform the services by submitting the company's profile, description of similar assignments, experience in similar conditions, availability of appropriate skills among staff or any other information which assist selection process etc.

Interested parties may obtain further information from the office of the Strategic Planning and Policy Manager, Tanzania Agricultural Development Bank (TADB), 4th Floor Acacia Estates, Plot No. 84, Kinondoni Road, P. O. Box 63372, Dar es Salaam from 0800 hours to 1600 hours from Monday to Friday except on Public holidays.

**Shortlisting**

A shortlist of eligible companies will be prepared on the basis of Expression of Interest submitted to TADB and will be communicated to all shortlisted firms in writing. Selection will be done in accordance with procedures set out in the Public Procurement Act No.7 of 2011 and the Public Procurement Regulation of 2011 (Amendment of 2016) of the United Republic of Tanzania.

Expression of Interest should be channelled through the Tanzania Electronic Procurement System (TANEPS) on **www.taneps.go.tz** within fourteen days from the date of publication of this advert.

**Late Submission**

Late submission of Expressions of Interest (EoI) shall not be accepted for evaluation irrespective of circumstances.

Toll free : 0800 110 120 | info@tadb.co.tz | www.tadb.co.tz | tadbtz

## Wanaoajiri wageni bila vibali waonywa

**Na Pendo Thomas, KIGOMA**

KAMISHNA Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala, amewaonya baadhi ya wananchi wa Mkoa wa Kigoma wanaohifadhi raia kutoka Burundi na kuwatumikisha mashambani pasipo kufuata taratibu za kisheria.

Makakala alitoa onyo hilo jana wakati wa ziara yake ya kikazi mkoani Kigoma ya kukagua maeneo yanayopakana na Burundi katika wilaya za Kibondo na Kakonko kwenye mipaka ya Muhange na Mkalazi.

"Tunatakiwa kuhakikisha suala la ulinzi na usalama linahimarika katika mikoa hii iliyo mipakani, hivyo sisi tutahakikisha tunasimamia," alisema.

Dk. Makakala alisema endapo taratibu rasmi zitatumika kuwaingiza raia hao nchini, itasaidia kuwafuatilia kama wamerejea nchini kwao baada ya msimu wa kilimo kupita na kama sivyo hatua za kuwafuatilia walikoelekea kufanyika.

Uingizwaji wa raia hao wa kigeni umekuwa ukihusishwa na vitendo vya uhalifu vinavyoripotiwa mara kwa mara katika mkoa wa Kigoma kwa kuwa baadhi ya wananchi wa Tanzania wamekuwa wakiwadhulumu, hivyo kurudi kulipa kisasi.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kakonko, Kanali Hosea Ndagala, alisema wilaya hiyo ina mipaka mikubwa ya wazi yenye zaidi ya kilomita 40, hivyo kuwaomba uhamiaji kuongeza nguvu kazi zaidi katika wilaya hiyo itakayowezesha kusimamia vyema.

Alisema wilaya hiyo ni ya mwisho kisha inakwenda mikoa mingine, hivyo raia wa kigeni wanaofanikiwa kupita katika eneo hilo wamekuwa wakienda katika maeneo mengine ya Tanzania ambayo utambuzi wa kuwabaini unakuwa mgumu.

Niyonkuru Protas, raia wa nchi ya Burundi, alisema wanalazimika kutembea umbali mrefu kutoka mpaka wa Muhange hadi Kakonko kufuata vibali vya kuingia nchi ya Tanzania kutokana na eneo la mpaka huo kutokutoa huduma hiyo hivyo kuomba usogezwaji wa huduma karibu.

"Tunapata shida kujieleza pale tunapokamatwa na polisi tukiulizwa kwa nini hatuna vibali wakati katika mpaka wa Muhange hakuna huduma hiyo," alisema.

# TRA yaja na kampeni 'mlango kwa mlango'

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imekusudia kuwafikia wafanyabiashara 3,500 katika kampeni ya elimu ya mlipakodi maarufu 'mlango kwa mlango'.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, Meneja wa Elimu ya Mlipakodi wa TRA kutoka makao makuu, Diana Masalla, alisema lengo la kutoa elimu hiyo ni kuwajengea uelewa wa wafanyabiashara na walipakodi masuala yanayohusu kodi. Alisema kampeni hiyo inalenga kuwaondoa hofu wafanyabiashara ili wasiwaone maofisa wa TRA kama ni watu wanaowakomoa bali lengo ni kuwa marafiki ili waweze kulipakodi kwa hiari yao wenyewe.

Maofisa hao wanatoa elimu hiyo na kusikiliza maoni ya wafanyabiashara kwa ajili ya kuboresha huduma za TRA na kuwakumbusha kulipa kodi stahiki na kwa wakati.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Philimon Sengati, alisema kwamba wananchi na wafanyabiashara wanapolipa kodi ndio kichwa cha uchumi wowote duniani.

Alisema kutokana na jitihada kubwa za serikali za kukusanya kodi, ndio maana miradi mikubwa inatekelezwa nchini kwa kuwa ni kodi za Watanzania wenyewe zinafanya kazi hiyo.

Dk. Sengati alisisitiza kwamba serikali inatumia gharama kubwa kuendeleza huduma za kijamii ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya, zahanati, barabara, madaraja na elimu bure kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Aliwataka maofisa wa TRA kuacha kutumia nguvu kwa ajili ya kukusanya kodi bali watumia elimu hiyo pamoja na lugha nzuri kwa wafanyabiashara hao.

"Sote tunafahamu umuhimu wa kodi katika maendeleo ya nchi yetu na ni ukweli usiopingika tumeona jinsi kodi inavyofanyakazi katika kipindi hiki cha serikali ya awamu tano inayoongozwa na Dk. John Magufuli," alisema Sengati.




Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), Mkoa wa Temeke, Alpha Amos (kulia), akitoa maelezo kwa wananchi wakati wa jukwaa la kusikiliza na kutatua kero za wananchi 'One Stop Jawabu', lililoandaliwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Temeke, katika Viwanja vya Zakhem, eneo la Mbagala, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mlipuko wa petroli waua na kujeruhi watano familia moja

**Na Steven William,** MUHEZA

MKAZI wa Mtaa wa Masimbani wilayani Muheza, Amiri Omari, amefariki dunia na wengine watano kujeruhiwa vibaya baada ya kuungua moto.

Tukio hilo limetokea juzi majira ya saa 6:00 usiku wakiwa wamelala ndani ya nyumba ya familia waliyokuwa wakiishi. Mkuu Mkuu wa Kituo cha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wilayani Muheza, Sajenti Masoud Mwagilo, alisema waliojeruhiwa kwa moto wako katika hali mbaya na wamelazwa katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Muheza.

Mwagilo aliwataja majeruhi kuwa ni Amiri Mohamed, Habiba Mohamed, Farida Waziri, Nurdini Mohamed, Hamza Mohamed na Ally Mohamed.

Akizungumzia chanzo cha tukio hilo, Mwagilo alisema ni kulipuka kwa petroli iliyokuwa imehifadhiwa ndani ya nyumba hiyo.

Alisema mmiliki wa nyumba hiyo, Omari, ambaye kwa sasa ni marehemu, alikuwa anafanya biashara ya kuuza mafuta ya petroli ndani ya nyumba yake kinyume cha sheria.

Mwagilo alisema mmiliki huyo aliwasha kibiriti ili avute sigara, huku watu wakiwa wamelala na baada ya kumaliza kuvuta sigara, alitupa kipisi karibu na madumu ya mafuta na yeye akaingia kulala.

Alisema baada ya kulala na kupitiwa na usingizi watu wote, kile kipisi kilikuwa kinawaka ndipo kikasababisha joto katika madumu ya mafuta kisha kulipuka ndani ya nyumba, hivyo watu hao kuungua vibaya, nyumba na mali zote kuteketea.

Kutokana na tukio hilo, mkuu huyo alitoa wito kwa wananachi kuacha mara moja kufanya biashara ya mafuta ya petrol ndani ya nyumba zao kwa kuwa ni hatari kwa maisha yao. Katika hatua nyingine, Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Mwanasha Tumbo, amepiga marufuku biashara hiyo kwenye makazi ya watu.

HABARI KITAIFA

## Serikali yakunwa usambazwaji wa zana kilimo

**Na Mwandishi Wetu, SUMBAWANGA**

WIZARA ya Kilimo imeridhishwa na usambazaji wa mbolea nchini unaofanywa na Kampuni ya Agricom Africa Limited kwa kupeleka vijijini matrekta na zana nyingine za kisasa.

Hayo yamebainishwa na Ofisa Mkuu wa Zana za Kilimo wa wizara hiyo, Godwin Mubi, akisema zana hizo ni bora na zitawasaidia wakulima kuzalisha mazao mengi na kuinua kipato cha mkulima.

Akizungumza kwa niaba ya wizara katika mafunzo yanayoendelea wilayani Kalambo, Mkoa Rukwa, Mubi, alisema wizara inatambua mchango wa Kampuni ya Agricom katika kuinua na kuboresha kilimo kwa kusambaza zana za kilimo katika maeneo mbalimbali nchini. Mkoa wa Rukwa kwa awamu ya kwanza umetengewa zaidi ya matrekta 17.

Alisema lengo la serikali ni kutumia kilimo kuinua maisha ya wakulima nchini kote, lakini tatizo ni kwamba wakulima wengi wana uelewa mdogo sana juu ya matumizi ya zana bora na uhusiano wa zana hizo katika kuinua uzalishaji wa mazao na uboreshaji wa maisha yao wenyewe.

"Agricom Africa ni moja wa wadau ambao wamekuwa wakiunga mkono juhudi ya wizara na serikali kwa ujumla katika kutekeleza mpango wa kuinua sekta ya kilimo awamu ya pili (ASDP II) kwa kuhakikisha zana za kisasa zinawafikia wakulima na wanajua matumizi yake. Tunawapongeza kwa kazi hii inayofanywa kwa manufaa mapana ya taifa letu," alisema Mubi.

Mubi alisema mafunzo yanayoendeshwa na kampuni hiyo yataondoa tatizo la uelewa mdogo wa wakulima juu ya matumizi ya zana za kisasa na kuwafanya wapende kutumia zana hizo. Amesema matumizi ya zana bora yataongeza uzalishaji mara tatu juu ya uzalishaji unaotokana na jembe la mkono.

"Takwimu zinaonyesha matumizi ya trekta kwa mkoa wa Rukwa ni asilimia 4 tu na asiliamia zaidi ya 80 wanatumia wanyama kazi na iliyobaki ni jembe la mkono. Hali hii ndio imefanya mafunzo haya yaanzishwe mkoani Rukwa," alisema Mubi na kuongeza kwamba Tanzania ina hekta 44 milioni zinazofaa kwa kilimo, lakini ni hekta 10.8 milioni tu ndizo zinalimwa kwa sasa.

Mkulima wa Kijiji cha Katete Wilaya ya Kalambo, Monica Mgala, alisema kijiji chao hakina trekta na kusema kwamba kijiji kikipata trekta uzalishaji utaongezeka.

Mkuu wa Ufundi wa Kampuni ya Agricom Africa, Philipo William, aliwahakikishia wakulima kwamba zana zote zilizopangwa zitawafikia kwa wakati katika msimu huu wa kilimo.

"Zaidi ya matrekta 17 yatakabidhiwa kwa vyama vya ushirika mwezi Oktoba na Mkuu wa Mkoa wa Rukwa. Kampuni yetu imejipanga vizuri katika kutoa huduma hiyo muhimu kwa wakulima kwa wakati," alisema William.

0000000

# Mgombea mwenza SAU awaahidi neema wanawake

**Na Yasmine Protace**

CHAMA cha Sauti ya Umma (SAU) kimeahidi kuwa kitawainua wanawake kimaendeleo ikiwa kitachaguliwa na kushika dola.

Mgombea mwenza wa urais wa Jamhuri ya Muungano kupitia chama hicho, Msatia Mussa, ndiye aliyebainisha hayo wakati wa uzinduzi wa kampeni za uchaguzi mkuu mwishoni mwa wiki, Gombo la Mboto, jijini Dar es Salaam.

Msatia aliwaomba wanawake wakiunge mkono chama chao na kwamba, kikiingia madarakani kitawaletea mabadiliko makubwa ya maendeleo.

Alisema, ilani yao inaeleza pia kuwa serikali yao itaondoa gharama pale mjamzito anapojifungua.

Kwa upande wake, mgombea urais wa Tanzania kupitia chama hicho, Muttamwega Mgaywa, alisema anazo sifa tatu ambazo zinamfanya awe rais wa Tanzania.

Amezitaja sifa hizo kuwa ni mzalendo, muadilifu na mwajibikaji. "Ninazo sifa tatu za kunifanya niwe mgombea urais na pia niwe rais kwa sababu sifa za rais ni tatu, ambazo ni uzalendo, uadilifu na uwajibikaji," alisema.

Aliongeza kuwa, mambo yaliyomo kwenye ilani ya uchaguzi ya chama hicho yanatoa kipaumbele katika kutokomeza adui ujinga, rushwa, maradhi pamoja na kuhakikisha huduma za afya zitatolewa bure kwa kila Mtanzania.

Aliongeza kuwa, ilani yao inalenga kutoa elimu bure kuanzia msingi mpaka chuo kikuu.

"Mbali na kusoma bure, tutawasaidia wanafunzi ambao wanataka kusoma nje ya nchi... watasoma kwa sababu zipo nchi ambazo zinawasaidia watu kupata elimu kupitia maarifa mbalimbali," alisema.

Alisema, ilani yao itasimamia pia katika utekelezaji wa walemavu wa viungo na vipofu kwa kuwawezesha vifaa, ambavyo watavitumia kwa kuwasaidia kuendana na ulemavu walio nao.

Alisema, ilani yao imejikita pia kuhakikisha kila Mtanzania anafaidi matunda ya nchi.

Alisema ili yote hayo yafanyike, aliomba apigiwe kuwa na makundi yote katika jamii.

Pia, alilitaka Jeshi la Polisi kutambua umuhimu wa kutoa askari kwa ajili ya kuwalinda wagombea, katika mikutano ya kampeni ambayo inaendelea nchi nzima.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Godfrey Mkamilo (wa pili kushoto), akitoa maelezo kuhusu zao la mchikichi kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerard Kusaya, alipotembelea kituo cha utafiti cha TARI cha Ilonga, wilayani Kilosa, mkoani Morogoro, jana. Kushoto ni Mkuu wa Kituo hicho, Dk. Joel Meliyo. **PICHA: FRANK KAUNDULA**

# Waandishi wakumbukwa bima ya afya

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) wazindua mpango wa huduma za matibabu kwa waandishi wa habari, ambapo jumla ya wanahabari 65 na wategemezi wao 20 wakiwa wamejiunga, huku kundi hilo likitakiwa kujiunga kwa wingi sambamba na kuelimisha jamii, kuhusu umuhimu wa bima ya afya.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mpango huo mkoani Mwanza, Mkuu wa Mkoa huo, John Mongella, alisema maendeleo yanaweza kuporomoka kama afya itakuwa dhaifu, kwani afya ni mtaji mkubwa katika maisha ya binadamu na inaleta tija katika maisha binafsi, familia, taasisi na taifa kwa ujumla, hivyo waandishi wa habari watumie fursa hiyo kujiunga na mpango huo wa bima, ili kuwa na uhakika wa matibabu.

"Hakuna mtaji mkubwa kwa binadamu kama afya, suala hilo ni nyeti sana katika muktadha wa maendeleo ya taifa, wanahabari ni kundi linalosahaulika sana na ni sekta muhimu hasa katika kipindi hiki, hivyo kupata bidhaa hii ambayo inamgusa moja kwa moja kupata huduma ya afya ni jambo jema ambalo limefanywa na NHIF, hivyo wanahabari muache ubahili... haiwezekani suala la afya yako mwenyewe kwa kutoa 100,080 kwa mwaka likawa jambo gumu, tusichukulie mzaha na jambo hili nitalivalia njuga," alisema Mongella.

Aliwataka kutilia mkazo suala la kuelimisha jamii kuhusiana na umuhimu wa bima, na kuwa amekuwa akiwaambia viongozi wenzake ni vyema wakatilia mkazo kuelimisha jamii kuhusiana na suala hilo, ambalo ni muhimu kwa afya na maendeleo ya taifa.

Mkurungezi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alisema lengo la mpango huo ni kutoa suluhu kwa wanahabari katika kukabiliana na gharama za matibabu, kwani wamekuwa wakishuhudia kundi hilo linavyopata shida, mmoja wao au mmoja wa wanafamilia anapougua, wanavyohangaika kugharamia matibabu.

"Hii ni kutokana na ukweli kwamba, kundi hili halikuwa na utaratibu maalum wa kuhudumiwa katika mfumo wa bima ya afya na hatimaye walikuwa wanajiunga wachache kupitia utaratibu wa kikoa, hivyo mfuko kwa kushirikiana na Umoja wa Klabu ya Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC) na Klabu za Waandishi za Mikoa tukiendelea kuwa na mikutano ya elimu kwa waandishi katika mikoa na tukaona kuna haja kwa kundi hili kuwa na utaratibu wake wa kujiunga na mfuko huu," alisema Konga.

Alisema kwa takwimu walizopewa vyama vya waandishi wa habari nchini vipo 28 vyenye wanachama 1,800, ambapo hadi kufikia Septemba 13, ni wanahabari 65 na wategemezi wao 20 wamejiunga, hivyo ameiomba UTPC kuchangamkia fursa hiyo, kwa kuwakumbusha na kuhakikisha wanachama wao wanajiunga na mfuko huo, kabla ya kuugua ambao itamlazimu kuchangia Sh. 100,080.

Rais UTPC, Deogratius Nsokolo, alisema kati ya klabu 28 zilizopo nchini ambao wanachama wake wamejiunga na mpango huo ni klabu 11 ikiwamo klabu ya Mkoa wa Kigoma 17, Mwanza 16, Mbeya 11, Shinyanga 11, Zanzibar 8, Dodoma 5, Dar es Salam 3, Rukwa 1, Simiyu 2, Katavi 2, huku akiziagiza klabu kuendelea kuhamasisha waandishi wa habari kujiunga na vifurushi hivyo hata kwa kuchangia fedha kidogo.

# Watumishi umma wapewa mafunzo ya teknolojia

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WATUMISHI 24 na wahandisi kutoka Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (MWTC), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Kampuni ya Mawasiliano Tanzania (TTCL Corp.) na Tume ya TEHAMA (ICTC) wametunukiwa vyeti vya kukamilisha mafunzo ya siku 9 ya teknolojia ya 5G.

Hii ni hatua nyingine thabiti iliyochukuliwa na Tanzania kuelekea kuimarisha uwezo wake wa kuhamia dijitali.

Katika mafunzo hayo ambayo yametolewa na Kampuni ya Huawei Tanzania yamehusisha kundi la kwanza la wataalamu wa Kitanzania, ambao wamechukua kozi muhimu ya teknolojia za redio za 5G na upelekaji wa mtandao, mahitaji ya wigo wa 5G na upangiliaji, modeli za biashara za 5G na usimamizi wa 5G.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi vyeti hivyo iliyofanyika jana jijini Dodoma, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Dk. Zainab Chaula, aliwapongeza wahitimu wa mafunzo hayo pamoja na Kampuni ya Huawei Tanzania akibainisha kuwa serikali imedhamiria kuongeza uwekezaji kwenye nyanja ya dijitali. "Tunahitaji kwenda na wakati na kujifunza maarifa na ujuzi wa kisasa ambao unakidhi mahitaji ya enzi hii ya dijitali na kuwa makini na mifumo ya kisasa ambayo inaweza kubadilisha au kuvuruga biashara na maisha yetu. Jambo la muhimu zaidi tunahitaji kuimarisha ustadi wetu kwenye TEHAMA kupitia mafunzo na uwezeshaji mpya ili kuendana na kasi ya mabadiliko, kukabiliana na changamoto na kuwahudumia watu wetu kwa ubunifu na ufanisi," alisema Dk. Chaula. Aidha, Dk. Chaula alisema mafunzo haya ni mfano mzuri wa jinsi taifa linavyoweza kufanikiwa kwa kufanya kazi na wadau binafsi wa kuaminika katika kuimarisha uwezo wake.

"Uwekezaji huu umekuja wakati muafaka kwa kuwajengea uelewa wa kidigitali watumishi wa umma, na kwa kiwango kikubwa itasaidia uboreshaji wa jukwaa la huduma za kiserikali kidijitali, moja wapo ya vitu vitatu muhimu vya Programu ya Dijitali ya Tanzania (DTP). Ni muhimu kwetu kukuza mazingira wazi na mfumo wa ikolojia ambapo kila mdau anaweza kushiriki, kuchangia na kufaidika nayo, ambayo itasababisha ukuaji endelevu wa sekta na maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini," alisema.

Alisema serikali inakaribisha washirika kama Huawei kushiriki zaidi katika majadiliano, kujenga uwezo na mashauriano ya sera juu ya jinsi ya kukabiliana na changamoto na kutumia fursa ya kuelekea uchumi wa kati, na kutoa mchango wao katika ustawi wa taifa kidigitali.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Huawei Tanzania, Damon Zhang, alisema tangu kuanza shughuli zake nchini mnamo mwaka 2007, Huawei Tanzania imejitolea kufundisha maarifa na ustadi wa TEHAMA kwa Watanzania, na wataalamu wote kwa kuwajengea uwezo na utaalamu wa kimataifa huku akihamasisha vijana kuanza safari ya masomo yanayohusiana na TEHAMA.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Dk. Zainab Chaula (katikati), akikabidhi cheti cha kuhitimu mafunzo ya teknolojia ya 5G kwa Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA Tanzania, Dk. Samson Mwela, wakati wa kutoa vyeti kwa wahitimu wa mafunzo hayo, jijini Dodoma. Anayeshuhudia ni Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Huawei Tanzania, Damon Zhang (kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Asasi zafagilia uchumi usio tegemezi

**Na Christina Mwakangale**

ASASI za kiraia zimesema kuwa ipo haja ya jamii husasani kizazi kijacho kujiandaa na uchumi usiokuwa tegemezi katika kujiletea maendeleo yao na taifa.

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa MediaSpace, Vicensia Fuko, wakati akifungua mkutano ulioshirikisha asasi za kirai, waandishi wa habari na wataalamu wa takwimu mtandaoni, jijini Dar es Salaam.

Alisema lengo la mkutano huo ni kupata mrejesho kutoka kwa asasi saba ambazo zilichaguliwa kushiriki katika mchakato 'Story Telling Challenge' ambao ulikuwa ni maalumu kwa asasi hizo kutoa elimu kupitia vyombo vya habari.

Fuko alisema ili jamii iondokane na umaskini ni wakati sasa wa serikali kuwa na mtaala maalumu wa kuwaandaa watoto kujitegemea kiuchumi.

"Sera ya kujitegemea inaweza kujengwa kwa watoto wetu ili kuondokana na dhana ya kutegemea kutoka kwa mtu. Hii itasaidia kupunguza utegemezi wa kiuchumi kutoka nje," alisema Fuko.

Alisema kwa sasa inaweza kuchukua muda katika maandalizi ya nchi kuwa na uchumi unaojitegemea na kusema jamii ianze kujiandaa kisaikolojia.

Fuko alisema kuwa mchakato huo ulilenga kutoa fursa kwa jamii ambazo zinafanya vizuri katika jamii na zinakosa jukwaa la kuelezea shughuli zao.

"Katika jamii kupitia ulimwengu huu wa mitandao pamoja na baadhi ya watu kutumia vibaya mitandao, lakini kuna asasi za kijamii ambazo wanafanya kazi nzuri lakini hawasiki 'platform' ni ndogo, Media Space tukaanzisha mradi huu ambao umesaidia asasi kufikisha ujumbe kupitia vyombo vya habari," alisema Fuko.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la ELIMISHA, Festo Sikagonano, alisema ushiriki wa asasi hiyo katika mchakato huo, umesaidia kupanua wigo wa shughuli zao kuelimisha jamii kutunza akiba katika kipato wanachoingiza kila siku.

"Kila familia au kila mmoja lazima uwe na bajeti ambayo unajua fedha fulani nitafanyia jambo hili la maendeleo, bila bajeti ni sawa na kukimbia bila kujua unakoelekea," alisema Sikagonamo.

## Wanavijiji wa Masasi wajijengea madarasa

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WANANCHI wa Kijiji cha Malika, Kata ya Malika wilayani Masasi mkoani Mtwara, wameamua kujitolea kujenga vyumba viwili vya madarasa na ofisi moja ya walimu katika Shule ya Msingi Malika ili kupunguza adha ya baadhi ya wanafunzi wanaosoma shule hiyo kusomea nje.

Hayo yalisemwa mjini Masasi na Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Malika, Yusuph Mohamed, alipokuwa akizungumza na gazeti hili, na kubainisha kuwa katika kijiji hicho watoto wake wanasoma katika Shule ya Msingi Malika ambayo ina upungufu wa vyumba vya madarasa.

Mohamed alisema kuwa kutokana na changamoto hiyo, wakazi wa kijiji hicho walifanya kikao cha serikali ya kijiji na kijiji kutoa wazo la vijiji vyote vya kata hiyo vikutane na kuona namna bora ya kuisaidia shule hiyo juu ya suala la kuanza ujenzi wa miundombinu yake.

Alisema wananchi hao waliamua kuchangishana fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na hatimaye kukusanya zaidi ya Sh. milioni 1.7 na kwamba upatikanaji wa fedha hizo ulitokana na maazimio ya wananchi hao ya kila mwananchi mwenye nguvu ya kufanya kazi atoe Sh. 5,000.

Alisema ujenzi huo tayari umeshaanza tangu Agosti mwaka huu na upo katika hatua ya msingi na kwamba wananchi hao pia wanashiriki katika hatua mbalimbali za ujenzi ikiwamo kubeba mchanga, mawe, kuchota maji na kubeba tofauli, lengo likiwa ni kufanikisha kukamilika kwa ujenzi huo.

"Baada ya kukusanya fedha za michango hii walizochanga wenyewe wananchi walianza na kununua jumla ya tofali zipatazo 1,294, ambapo tofali hizo zimeshaanza kutumika katika ujenzi huo wa vyumba vya madarasa shuleni hapo," alisema Mohamed.

John Lisombe, mkazi wa kijiji hicho, alisema wameamua kujitolea kujenga vyumba vya madarasa baada ya kuguswa na watoto wanaosomea nje.

Naye Agnes Kasembe, alisema wao kama wananchi wanatambua kuwa serikali inafanya mambo mengi ya kimaendeleo hivyo wananchi pia wanawajibu kusaidia jitihada hizo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi, Changwa Mkwazu, aliwapongeza wananchi hao kwa kuamua kusaidiana na serikali katika kuleta maendeleo.

## Kwa sheria hizi mlungula unapitaje uchaguzi mkuu? (2)

Ukurasa 12





siasa
JUMATANO SEPTEMBA 16, 2020
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

Ukurasa 13

## Oktoba 28 mwananchi unaachaje kupiga kura?

# Kwa ilani hizi Tanzania isiyo na magonjwa inawezekana

- Zahanati moja kwa watu 1,000...ACT.
- Kutibu wagonjwa KITEHEMA ...SAU

**Na Sabato Kasika**

WAKATI huu wa kuelekea uchaguzi mkuu mambo yanayowabana Watanzania ni pamoja na changamoto za huduma za afya, upatikanaji elimu bora na maji safi na salama. Masuala hayo yanaelezwaje ndani ya ilani za vyama?

Wagombea wanapoendelea kunadi sera na mikakati na mipango yao majukwaani, Nipashe inaangaza ahadi zilizomo kwenye ilani za vyama zenye kuboresha afya kwenye vyama vya Sauti ya Umma (SAU), CUF, ACT Wazalendo, CCM na CHADEMA.

Kwa kuwa ahadi ndani ya ilani hizo ni nyingi lakini uboreshaji wa afya ni suala la kipaumbele na kila chama kinatambua hilo.



Tiba mtandao ni miongoni mwa mikakati inayotajwa na wanasiasa kwenye kuimarisha afya. **PICHA:MTANDAO.**

### MKAKATI WA SAU

SAU, katika ilani yake, inaitaja afya kama msingi wa kila kitu na kwamba bila afya bora mtu hakuna uzalishaji na kuchangia uchumi wa taifa.

Chama kinakiri sehemu za kupata matibabu ni chache hivyo kusababisha wananchi kusafiri umbali mrefu kwa ajili ya kufuata huduma za afya, tena hawana uhakika wa matibabu kwa vile hawana pesa.

"Upatikanaji dawa hauridhishi , kuna upungufu mkubwa wa wataalam hasa vijijini, hivyo mkakati ni kujenga zahanati kila kijiji." Aidha, kinakusudia kujenga kituo cha afya kila kata kitakachohudumia mama na mtoto, kujenga hospitali kila wilaya na sita za rufani kwa kila kanda zenye kutiba saratani.

SAU itatumia tiba mtandao (telemedicine) inayofanyika kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kutibu na kutoa matibabu bure kwa kila mtu.

### CUF IMEJIPANGAJE?

Yapo mengi ambayo ilani ya CUF inataja kuhusu afya, ukurasa wa 136 inaainisha changamoto za huduma hiyo na kueleza kuwa hospitali nyingi za serikali zina uhaba mkubwa wa wagonjwa kwa sababu hawawezi kumudu gharama za matibabu.

Ilani inasema, kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo la afya, serikali ya umoja wa kitaifa chini ya CUF itatenga asilimia 15 ya bajeti ya serikali kuboresha huduma za afya. Miongoni mwa yatakayofanyika ni kutoa, huduma za msingi za afya bure na zitakuwa ni haki ya kila Mtanzania.Mkazo utakuwa kukinga pamoja maradhi na chanjo.

Aidha, virutubisho vitaongezwa katika vyakula hasa unga wa mahindi, wa ngano na kutoa elimu ya afya kwa kina.

"Tiba ya saratani, kisukari, figo na shinikizo la damu na baadhi ya maradhi ya kuambukiza kama vile malaria, kifua kikuu,Ukimwi na minyoo, itapatikana bure."

Kadhalika ili kufidia pengo vyanzo vingine vitachangia huduma za afya japo serikali itatenga asilimia 15 ya bajeti.

Serikali itaboresha utaratibu wa bima ya afya, waajiri watatakiwa kuwakatia bima wafanyakazi na kuwawezesha wanachama wa mpango huo kupata huduma popote nchini.

### CCM NAO VIPI?

Kuanzia ukurasa wa 124 wa ilani yake, CCM inaelezea mengi ambayo serikali imefanya miaka mitano iliyopita na kutaja mkakati mingine ya miaka mitano.

Chama kinaahidi kuweka kipaumbele sekta ya afya kwani inagusa maisha ya Watanzania na ustawi wa taifa na kwamba serikali itaendelea kutoa bure huduma za afya ya mama na mtoto, kupunguza vifo vya kinamama wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Jingine ni kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na pia CCM itaweka mazingira kwa sekta binafsi kujenga viwanda ili kuzalisha dawa, vitendanishi na vifaa tiba kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini ili kupunguza mzigo kwa serikali wa kuagiza bidhaa hizo nje.

Kufikia 2025 serikali itaongeza vituo vya kutolea huduma za afya kwa asilimia 20 ya vituo 8,446 vilivyopo sasa.

Kadhalika itaimarisha mifuko ya bima za afya NHIF na CHF ili kuwezesha kila mtu kuwa na bima hiyo.

### CHADEMA WANA LIPI?

Ukarasa 42 wa ilani una taarifa za afya zinazosema kwa kushirikiana na sekta binafsi itawapa wananchi wote huduma bora ya afya, itajenga, kuendeleza na kutumia miundombinu ya afya kiubia baina ya sekta ya umma na binafsi (PPP)

Itaongeza udahili wa wanafunzi wa mafunzo ya watendaji wa afya ili kukidhi mahitaji ya jamii kwa mfumo wa ubia sekta binafsi na ya umma (PPP) lakini mbia mkuu ni serikali.

Inaahidi kutoa motisha kwa watendaji wa sekta ya afya kwa nafasi zao, kukuza matumizi ya teknolojia kwenye afya.

Ilani hiyo inasema, serikali ya Chadema itaimarisha Baraza la Taifa la Utafiti wa Kitabibu kwa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya utafiti wa kitabibu na kutoa kwa wakati.

Ilani inaahidi kusajili taasisi za ndani za utafiti wa kitabibu, tiba asili na tiba mbadala ili kuboresha sekta ya afya nchini.

Aidha, itahimiza sekta binafsi kuwekeza katika kuanzisha huduma ya usafiri kwa wagonjwa katika hospitali za umma, kuanzisha mchakato wa kujitathimini kwa wahudumu wa afya kwa ajili ya maisha yao viwango vya maslahi na ubora kwa ajili ya utoaji huduma.

### ACT-WAZALENDO

Masuala ya afya yanatajwa kuanzia ukurasa wa 22 sehemu ya 3.2.1, chama kikiahidi kusimamia ujenzi wa zahanati mijini na vijijini kufikia lengo la kuwa na zahanati moja kwa watu 1,000.

Itajenga na kuboresha hospitali za mikoa ili ziwe za kisasa, zenye kukidhi viwango vya kimataifa, ikiwa ni pamoja na kuwekeza na kuboresha uchunguzi wa maradhi.

Itafanya uwekezaji mkubwa wa miundombinu ya afya kwa kuwa na hospitali kubwa tatu za kanda zenye hadhi, uwezo na viwango vya kimataifa zikijengwa Mara, Ruvuma na Singida.

Sehemu ya 3.2.2. ya ilani inasema, itawezesha wafanyakazi wa afya hasa kwenye ngazi ya zahanati kutoa elimu ya afya kwa umma wakishirikiana na viongozi wa serikali za mitaa, vitongoji na vijiji, ili kuzuia maradhi.

# Kwa sheria hizi mlungula unapitaje uchaguzi mkuu? (2)

Na Gaudensia Mngumi



UCHAGUZI ni mchakato unaosimamiwa na sheria ili kudhibiti udanganyifu na mbinu mbalimbali za kuwavuta wapigakura iwe kuwaahidi ajira, nyadhifa na hata misaada ya pesa.

Kila kinachopokelewa wakati wa uchaguzi ili kujenga mazingira ya kupata kura au kupata upendeleo wa aina yoyote huchukuliwa kuwa ni rushwa. Ndiyo maana kuna sheria zinazokataza kutoa hongo, lakini kwenye uchaguzi hali ni shwari? Wagombea hawawalipii nauli wapigakura?

Vipi taarifa kuwa mgombea fulani anawaandalia wapigakura au wajumbe chakula na vinywaji? Sheria zinasemaje? Makala hii iliyoanza tangu wiki iliyopita inaangaza sheria, uwapo wa rushwa na pengine hatua za kuchukua kuidhibiti.

Kaulimbiu ya Tanzania tangu uhuru mwaka 1961 ni kupata maendeleo na ili kuendelea unahitajika watu ambao ni nguvukazi, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Ndiyo maana uchaguzi unafanyika ili kuwapata viongozi bora. Hivyo kwa mujibu wa sheria ni lazima uongozi huo asitokane na rushwa.

Sheria zinalenga kuwezesha uchaguzi uwe huru, wa haki, wa wazi na unaoaminika.

Baadhi ya sheria hizo ni ile ya Gharama za Uchaguzi ya Mwaka 2010 inayokataza kutoa au kusaidia kuwezesha kupata ajira au wadhifa sehemu za kazi kwa lengo la kufanikisha kupigiwa kura.

Inakataza pia kutoa zawadi, mkopo, msaada, ahadi au kitu chochote au kuingia makubaliano na kufanikisha uteuzi kutokana na zawadi, mkopo, msaada, ahadi au makubaliano yaliyoingiwa baina ya mgombea na wapigakura.

Aidha, Sheria ya Gharama za Uchaguzi namba 6 ya Mwaka 2010 inawakataza wagombea kulipa au kuagiza kulipwa fedha ili zitumiwe kwa ajili ya hongo kupiga kura za maoni au uchaguzi wowote.

Halikadhalika, inaweka jinai kupokea au kukubali fedha, zawadi, mkopo, msaada, ahadi, wadhifa au kitu chochote chenye thamani ili raia apige kura.

Sheria hiyo pia inakataza kutoa au kupokea shukrani baada ya uchaguzi, lakini haishii hapo inazungumzia malipo haramu. Kifungu cha 22 (a) na (b) kinasisitiza kuwa ni kosa kwa yeyote kwa njia ya rushwa kutoa, kuandaa, kulipa kwa ujumla au sehemu, gharama ya kutoa au kuandaa chakula, kinywaji, burudani au mahitaji ya au kwa ajili ya mtu yeyote kwa madhumuni kumshawishi raia kupiga kura au kuzuia kupiga kura katika mchakato wa uchaguzi.

### KUKATAZA KUTOA USAFIRI

Sheria hiyo inakataza kusafirisha wapigakura, yote yakianishwa kifungu cha 23 (1) (a), (3) na 23 (4): Inakatazwa mgombea au wakala na chama cha siasa kuwasafirisha wapigakura kwenda au kutoka kituoni kwa kukodi gari, chombo cha majini, mnyama au usafiri wa aina yoyote ile kwa kuwatolea nauli.

### MAKATAZO MENGINE

Kununua au kuuza kadi ya mpigakura ili kumzuia kupiga kura. Aidha, inakataza kutoa rushwa kwa mgombea ili kumshawishi ajitoe kwenye kugombea.

Sheria pia zinakataza mgombea kuomba au kupokea rushwa ili ajitoe kwenye mchakato. Pia kutoa rushwa ili kuteuliwa kugombea, kuomba au kupokea rushwa ili kumteua mgombea.

Kushawishi au kupokea rushwa ili kumpigia kura mgombea fulani au kuacha kupiga kura, yote yanakatazwa na sheria hiyo.

### MAKOSA YA RUSHWA

Makosa ya rushwa katika uchaguzi yanatajwa na sheria hiyo kuwa ni kutoa mlungula kwa mpigakura ili kumshawishi kumpigia kura mgombea fulani au kuacha kupiga.

Kutoa takrima, hongo ili kupindisha sheria, kanuni na taratibu za uandikishaji wapigakura, uendeshaji wa kampeni, upigaji wa kura au utangazaji wa matokeo ya uchaguzi.

Makosa mengine ni kuomba au kupokea hongo ili kupindisha au kufumbia macho sheria, kanuni na taratibu za uandikishaji wapiga kura, uendeshaji wa kampeni, upigaji wa kura au utangazaji wa matokeo ya uchaguzi.

Kutoa hongo, kukirimu au kushawishi kunakohusisha wajumbe au maofisa wa usimamizi wa uchaguzi.

Ofisa Habari wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ( TAKUKURU), Kirumbi Matai, anasema taasisi hiyo ndiyo inayodhibiti, kuzuia na kupambana na rushwa kwa kuuelimisha umma athari ya rushwa kwenye uchaguzi na faida za kuwa na uchaguzi huru.

Aidha, anasema wananchi wanafahamishwa na kuelimishwa kuhusu kuthamani kura, nafasi na wajibu wa mwananchi kukataa na kukabili vitendo vya rushwa katika uchaguzi.

"Tunafanya utafiti wa mchakato wa uchaguzi kanuni na taratibu kubaini mianya ya rushwa na kupendekeza jinsi ya kuiziba." Anasema Matai.

### KWANINI KUNA RUSHWA?

Licha ya sheria, TAKUKURU na wadau wa uchaguzi kuwaelimisha wananchi kuhusu thamani ya kura kuwa ni mkataba wa kumuajiri mwanasiasa kwa miaka mitano, wananchi wanaendelea kuthamini 'kitu kidogo'.

Kura inathaminishwa na bidhaa inalipwa kwa njia ya rushwa inayotolewa kwa mpigakura. Wengi wanapokea khanga, fulana, madera, chakula, fedha bila kujua kuwa thamani ya kura ni kubwa isiyoweza kupimika.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, idara ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma, Sabatho Nyamsenda, anasema kuwapo kwa rushwa kwenye uchaguzi ni matokeo ya mfumo wa kiuchumi wa ubepari 'neo liberalism,' unaogeuza kila kitu kuwa bidhaa ikauzwa na kununuliwa sokoni na kwamba hata uchaguzi pia hugeuzwa kuwa gulio la kisiasa, ambapo mwanasiasa ndiye mteja na mpiga kura ndiye muuzaji na bidhaa inayouzwa ni kura.

"Kwa maana hiyo, kura hupoteza thamani (use value) na kubakia kuwa bidhaa yenye bei au exchange value, tatizo hili lipo katika hatua zote za uchaguzi, tangu kura za maoni ndani ya vyama vya siasa hadi katika uchaguzi mkuu wenyewe.".

Kwa hiyo licha ya kuwapo sheria suala la "mkono mtupu haulambwi" au "penye udhia penyeza rupia." Ni mambo yanayotawala fikra za wapigakura ambao wanaamini kuwa ni lazima kutoa kitu ili mtu apate kura yake.

### UNAHITAJIKA UTAFITI

Pengine ni wakati wa wadau kufanya utafiti na kuona kitu gani kinachowafanya wapigakura na wengine wanaoshiriki uchaguzi kuona kuwa ni lazima wapate pesa au kitu kwanza ili wamchague mgombea? Kwanini wajione kuwa wanahitaji kulipwa? Wawe wajumbe wa kupitisha majina ya wagombea, wahamasishaji wapigakura na makundi mbalimbali ya kijamii ni sababu zipi zinazowavuta watake kupewa pesa na vitu na wagombea wa uongozi?

Huenda marupurupu manono na malipo makubwa wanayopata wanasiasa yakawa sababu ya kuwafanya wapigakura kuona kuwa wagombea ni mabilionea wanaoweza kuwapa pesa na vitu kwa vile kuwa mwanasiasa ni sawa na kumiliki kisima cha mafuta au utajiri mkubwa.

# Oktoba 28 mwananchi unaachaje kupiga kura?




Mchakato wa uchaguzi ukiendelea katika moja ya vituo vya kukusanya na kuhesabu karatasi za kura. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Reubeni Lumbagala**

OKTOBA 28 ni siku ya uchaguzi mkuu ambayo wananchi waliojiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura watapata fursa ya kuchagua viongozi kuanzia, rais, wabunge na madiwani ili kuwaongoza katika kipindi cha miaka mitano ijayo inayoanza Novemba 2020 hadi Oktoba 2025.

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, uchaguzi mkuu hufanyika mara moja kila baada ya miaka mitano. Kwa hiyo kutokana na umuhimu wa uchaguzi katika kuleta maendeleo ya nchi wananchi wamekuwa wakielimishwa kuhusu umuhimu wa kushiriki katika mchakato huo wa kidemokrasia lakini wakitakiwa kwanza kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapiga kura, wanasikiliza sera za wagombea na hatimaye kupiga kura kwa wagombea wanaokidhi vigezo ili kushirikiana na wagombea hao katika jitihada za kujiletea maendeleo katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Kwa muda mrefu, wadau wa kisiasa, viongozi wa dini na wananchi wamekuwa wakipendekeza mabadiliko ya siku ya kufanyika uchaguzi ambao kwa miaka mingi, umekuwa ukifanyika Jumapili.

Kuchagua viongozi siku hiyo kulikuwa kukiwakwamisha baadhi ya wananchi walioshindwa kuchagua viongozi kutokana na kushiriki ibada hasa kwa wapigakura Wakristo.

Kukipa heshima na umuhimu na kuhakikisha ushiriki wa wananchi katika uchaguzi mkuu lakini pia serikali kutambua na kuheshimu imani za dini za wananchi na mapendekezo yaliyokuwa yakitolewa na wadau mbalimbali, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ilitangaza Oktoba 28, 2020 ambayo itakuwa siku ya Jumatano kuwa ndiyo iliyotengwa kwa ajili ya kupiga kura.

Jumatano pia itakuwa ni siku ya mapumziko kitaifa ili kuondoa kikwazo kilichokuwa kikikwamisha wananchi kupiga kura.

Kufanyika kwa uchaguzi siku ya Jumatano na ambayo pia haitakuwa na kazi kunatoa nafasi kwa wafanyakazi kuwahi kwenye vyumba vya kupigia kura.

Hatua ya NEC kubadili ratiba na mazoea ya miongo kadhaa ya kupiga kura Jumapili inaonyesha namna ambavyo uchaguzi ambao ni mchakato wa kidemokrasia ulivyopewa heshima ya aina yake ili kuhakikisha kila mmoja anashiriki ili kuchagua viongozi bora kwa maendeleo endelevu. Ndiyo maana swali hili ni kwa kila mmoja unaachaje kupiga kura Oktoba 28, 2020?

> “Kutokana na Oktoba 28 kutengwa kuwa siku ya kitaifa, itashangaza kama wananchi watashindwa kuitumia fursa hiyo muhimu kuhakikisha kuwa wanajitokeza kwa wingi katika vituo vya kupiga kura ili kutimiza haki yao ya kikatiba ya kuchagua vongozi.

Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere katika uongozi wake alitaja mambo manne ambayo yanachangia nchi kupata maendeleo nayo ni watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

Uongozi bora unapatikana kwa kuwa na uchaguzi wa kumchagua rais, mbunge, mwakilishi na diwani ili kuliongoza taifa katika kupata maendeleo hivyo wananchi wana wajibu wa kushiriki kikamilifu katika kupiga kura ili kupata viongozi bora.

Hawa ndiyo wanaohitaji ili pamoja na watu, ardhi na siasa safi Tanzania isongembele na kuondokana na maadui watatu ambao ujinga, umaskini na maradhi.

Kwa sasa Tanzania imeingia kwenye uchumi wa kati ni kazi ya uongozi bora na jitihada ya kuondoa umaskini, ujinga na maradhi na kulipandisha chati taifa.

Itakuwa ni jambo la kushangaza kama wananchi wanahitaji uongozi bora bila kushiriki kuwachagua kupitia sanduku la kura siku ya uchaguzi mkuu Oktoba 28, 2020.

Njia pekee ya wananchi kupata viongozi bora na hatimaye kutamalaki kwa kazi wanayoitaka ni kuwapigia kura wagombea bora wenye mwelekeo wa kuleta mabadiliko na ustawi wa wananchi badala ya kuendeleza siasa za kuchumia tumbo.

Uchaguzi Mkuu huu unatarajiwa kugharimu bilioni 331.7 ambazo zitagharamiwa na serikali kwa asilimia 100 katika kuandaa na kuendesha mchakato huo unaowahusu Watanzania wote.

Kwa mujibu wa NEC takribani wananchi milioni 29.2 wanatarajiwa kupiga kura za kuchagua madiwani, wawakilishi, wabunge na rais.

Bilioni 331.7 ni fedha zinazotolewa na serikali kupitia Mfuko Mkuu wa Hazina kwa kuzingatia kifungu cha 122 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi. Hizi ni fedha nyingi ambazo wananchi wanapaswa kuzithamini kwa kuhakikisha kuwa wanashiriki kikamilifu katika kuchagua viongozi bora.

Taarifa za NEC zinasema vituo 80,155 vya wapiga kura vimetengwa huku kituo kimoja kikitarajiwa kuhudumia wananchi 500.

Kero zinazowakabili wananchi katika maeneo mbalimbali kama vile ukosefu wa maji, upungufu wa vyumba vya madarasa, changamoto za nishati ya umeme, miundombinu mibovu na ukosefu wa masoko ya bidhaa zinaweza kutatuliwa wakiwapo viongozi bora wenye wito wa kuwatumikia wananchi na wapigakura wao.

Hivyo basi, ushiriki wa wananchi katika kuchagua viongozi bora ni njia ya kuelekea kuzipatia ufumbuzi kero hizo. Lawama na malalamiko dhidi ya viongozi hazitasaidia kupata uongozi makini badala yake wananchi washiriki kupiga kura Oktoba 28 ili waweze kupata wa kuwaongoza wanaokidhi matakwa ya Watanzania.

Kutokana na Oktoba 28 kutengwa kuwa siku ya kitaifa, itashangaza kama wananchi watashindwa kuitumia fursa hiyo muhimu kuhakikisha kuwa wanajitokeza kwa wingi katika vituo vya kupiga kura ili kutimiza haki yao ya kikatiba ya kuchagua vongozi.

Wagombea wanaoendelea kujinadi kuomba kura kwa wananchi, wahakikishe kuwa agenda ya kutetea na kusimamia maslahi ya wananchi inakuwa ni namba moja. Watu wanataka maendeleo, hivyo bila kusimamia maslahi ya wananchi, maendeleo hayawezi kufikiwa. Kila mwananchi aliyejiandikisha aweke ratiba zake ili Oktoba 28, aweze kushiriki zoezi muhimu la kupiga kura. Ikumbukwe kuwa uchaguzi mkuu unafanyika mara moja katika kipindi cha miaka mitano.

Kama huo ndiyo utaratibu kufanyika katikati ya Juma huku siku hiyo ikifanywa kuwa ya kitaifa na ya mapumziko, Watanzania wasipange kukosa kupiga kura ni muhimu kwa maendeleo ya taifa lao.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Sekondari ya Mlali iliyoko Kongwa mkoani Dodoma.***

***Maoni: 0765-409249.***

# MPIGA FILIMBI MARIA

• Msichana tishio anayeongoza kuung'oa udikteta wa Belarus

Na Ani Jozeni

PENGINE ni nadra kuwaona kinamama wakiongoza mapinduzi kwenye mataifa yao, hata hivyo zama zinabadilika Maria Aleksandrovna Kolesnikova sasa ni kiongozi wa kumtoa rais ikulu.

Mwanasiasa huyo ambaye ni mwanamuziki tena mpiga filimbi kitaaluma aliyezaliwa miaka 38 iliyopita ni tishio kwa ikulu ya nchi yake, baada ya kushiriki kikamilifu kwenye maandamano yasiyokwisha ya kuing'oa serikali ya kiimla ya Belarus.

Maria Kolesnikova anasikika duniani kote akiwa mjumbe na kinara wa kamati ya uratibu ya maandamano ya kumng'atua madarakani Rais Alexander Lukashenko wa Belarus.

Mtawala huyo alitangazwa kuwa mshindi kwa asimilia 80 ya kura wakati takriban kila mpiga kura aliyekuwa anaongea na mwenzie au anafahamu hisia zilizopo katika mtaa wake au mji alikuwa na uhakika kuwa Lukashenko hakupata watu waliompigia kura.

Kiongozi anayetakiwa kuondoka ikulu amedumu madarakani tangu mwaka 1994 akiwa ni masalia ya Urusi ya zamani iliyokuwa ikijulikana kama Muungano wa Jamhuri za Kisovieti - USSR.



### CHIMBUKO LA MARIA

Msichana huyo alizaliwa Aprili 24, 1982 na kukulia jijini Minsk, mji mkuu wa Belarus na kitovu cha maandamano hayo kwa mujibu wa taarifa zinazosambazwa hivi sasa mitandaoni, anataka kuingia ikulu.

Maria anatokea kwenye familia yenye uwezo kifedha, kwani wazazi wake ni wahandisi kitaaluma na alisoma katika shule binafsi alipomaliza sekondari, akaanza kujifunza muziki akibobea kwenye kupiga filimbi.

Alianza kushirikii katika maonyesho ya kikundi cha muziki cha taifa cha National Academic Concert Orchestra cha nchi hiyo na kumaliza masomo yake kama mpiga filimbi na muongozaji orchestra.

Alipofikisha miaka 25 Chuo Kikuu cha Muziki na Sanaa za Maonyesho cha Stuttgart nchini Ujerumani, akiwa amefaulu katika muziki wa zamani na wa kisasa mwaka 2012.

Kuanzia wakati huo Maria akaanza kuratibu miradi ya ushirikiano wa kitamaduni kati ya Ujerumani na Belarus na mwaka 2017 akashiriki kuanzisha kikundi cha fani na sanaa. Hadi mwaka jana alikuwa Mkurugenzi wa Sanaa wa Klabu ya OK 17 ya jijini Minsk.

Mwaka 2020 ulikuwa wa uchaguzi akaanza kuongoza kwaya tofauti.

### KUINGIA SIASA

Mei mwaka huu anajitosa kwenye kampeni ya kutiania urais ya Viktar Babaryka na kuteuliwa kuwa meneja wake. Babaryka alikamatwa na kupigwa marufuki kushiriki uchaguzi mkuu, hivyo Kolesnikova na Veronika Tsepkalo wakajiunga na kampeni ya Sviatlana Tsikhanouskaya, mwanamke mgombea urais ambaye alianza kupata umaarufu kwa kuchukua nafasi ya mumewe aliyezuiliwa kushiriki uchaguzi pia.

Sviatlana Tsikhanouskaya ni mwanamama kijana pia mwenye miaka 37 na mwalimu wa zamani wa Kiingereza, hali inayomfanya apate urahisi wa kujieleza katika vyombo vya habari vya kimataifa wakati alipokimbilia nje ya Belarus.

Licha ya kwamba alikuwa hajulikani kisiasa alipoingia ulingoni kuziba nafasi ya mumewe Mei mwaka huu, wanaompinga Rais Lukashenko hawakupata taabu kuelekeza kura zao kwake ndiyo maana 'ushindi wa kishindo' wa Lukashenko ulipotangazwa maandamano yalianza mara moja.

> Alianza kushirikii katika maonyesho ya kikundi cha muziki cha taifa cha National Academic Concert Orchestra cha nchi hiyo na kumaliza masomo yake kama mpiga filimbi na muongozaji orchestra.

### HARAKATI ZAIDI

Ilikuwa ni suala la kuangaliana machoni na kujua kuwa hakuna hata mtu mmoja aliyepiga kura kumuunga mkono Lukashenko, kati ya watu 10 au 20 wanaoongea na siyo rahisi kupata watu wanaosema kuwa idadi inayoweza kukaribia nusu ya wapiga kura ilimuunga mkono.

Hivyo maandamano yakaanza kutaka uitishwe uchaguzi mwingine ambao utakuwa huru, haki wenye unaoaminika, unaosimamiwa na waangalizi kutoka nchi za Ulaya.

Ni wakati wa kuelekea kupiga kura ambako Maria Kolesnikova alijiunga na kamati ya watu saba ya uendeshaji wa kampeni ya Tsikhanouskaya.

Kuanzia Agosti 20, Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Belarus akafungua kesi ya jinai dhidi ya wajumbe wa kamati hiyo ya uendeshaji maandamano, baada ya matokeo ya 'ushindi wa kishindo' kutolewa.

Maelezo ni kuwa kamati 'inajaribu kukamata mamlaka ya nchi, kuhatarisha usalama wa taifa.'

Mwanzoni mwa mwezi huu, Maria Kolesnikova ameunda chama kipya cha siasa akikiita Razam yaani 'Pamoja' au Rassemblement kwa Kifaransa, kujiendesha nje ya kamati ile ya chama kilichoshiriki uchaguzi mkuu.

Ilieleweka ni jitihada kubadilisha majina kuondoa kisingizio kuwa chama kilichoshiriki uchaguzi kinadai kuwa kimeshinda hivyo kinaendesha maandamano kutwaa mamlaka ya nchi.

Inakuwa ni kikundi kipya cha siasa kisicho na uhusiano na upigaji kura au wagombea katika uchaguzi mkuu ila kinasisitiza urudiwe.

Hatua hiyo, haikumwondolea masahibu ya kisiasa Maria Kolesnikova kwani polisi sasa wanatafuta viongozi wa waandamanaji na hakuna cha chama kipi cha siasa au kamati ya matayarisho.

Wiki iliyopita Septemba 7, Maria Kolesnikova akakamatwa na polisi waliovaa kininja ili kuficha nyuso, akiwa jijini Minsk, familia yake ikatoa taarifa vyombo vya usalama na katika vyombo vya habari kuwa hajulikani alipo ila siku iliyofuata akakamatwa karibu na mpaka wa Ukraine, vyombo vya usalama vikadai kuwa alikuwa akijaribu kutoroka alfajiri saa 10 akiwa na wasaidizi wawili wanaume.

Taarifa hizo hata hivyo zilikanushwa na ikaelezwa kuwa alichana hati yake ya kusafiria wakati utawala huo ukitaka kumsukuma nje ya mpaka aingie nchi nyingine inavyoelekea kwa madai kuwa ni raia wa Ukraine zaidi.

Wasaidizi wake wengine wawili katika kamati hiyo ya uratibu wa maandamano walikamatwa Septemba 9 na watu hao hao wanaoficha nyuso zao na Jumamosi iliyopita Septemba 12, mwanamama Maria Kolesnikova alihamishwa kutoka kituo cha kizuizini cha Minsk kupelekwa kituo kingine kinachosemekana ni cha muda, huko Zhodino.

Mizunguko na jitihada hizo za dola zinaonyesha mpiga filimbi huyo sasa ni kiongozi halisi, siyo tu kwamba ni mwanakamati katika kampeni ya Tsikhanouskaya ila ni kiongozi mwenza kikamilifu.

Ndiyo mgongano kimantiki wa ukandamizaji, kuwa unavyozidi kuswaga viongozi waliopo, ndiyo unazidi kuunda wengine wenye nguvu na kukubalika zaidi kiasi kwamba hata waliokuwa wanaamini utawala una nia njema, wanapatwa na shaka.

**MITANDAO**





# Mfumo majitaka bado tatizo nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imesema mamlaka za maji 11 kati ya 26 zinazotoa huduma kwenye mikoa ya Tanzania Bara, ndizo zenye mtandao wa majitaka.

Kutokana na hali hiyo, mamlaka hiyo imeandaa mwongozo wa kuondoa majitaka na takatope kwenye maeneo yasiyo na mtandao wa majitaka.

Mkurugenzi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa EWURA, Mhandisi Exaud Maro, aliyabainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kuwajengea uwezo watumishi kutoka kwenye mamlaka za maji mikoani na miradi ya kitaifa kuhusu mwongozo huo.

Mhandisi Maro alisema huduma ya majitaka inazalishwa kwenye makazi, lakini hakuna mfumo wa kuondoa maji taka na kwamba katika mamlaka hizo 11 si kaya zote zimeunganishwa na mfumo.

Alisema kwenye maeneo hayo, bado kuna vyoo vya shimo ambavyo uchafu ukifika hatolewi na kuelekeza mamlaka hizo kuwa na mfumo wa ufuatiliaji endelevu ili kaya ziwe na mifumo midogo midogo ya uchakataji maji taka.

"Pale ambapo kuna shimo la choo halafu hamna mfumo wowote wa kuchakata yale majitaka ili yafae kwenda kwenye ardhi, hapa tunapata kero sana ya uchafuzi wa maji chini ya ardhi na hii ni kwa vyoo vya shimo ambavyo havina. Mfumo huu wa kuchakata uchafu wa mwanadamu ili kufaa kuingia kwenye ardhi au maji yanayotiririka," alisema. Alisema topetaka linazalishwa baada ya utaratibu wa kibailojia wa kuondoa uchafu katika kinyesi cha binadamu. Mwongozo huo unaelekeza namna ya kutumika bila kuleta athari.

Alitoa wito kwa jamii kuhakikisha kuwa na choo bora ili kuondoa maji taka eneo la makazi ili kutopata maradhi.

Kuhusu mafunzo hayo, Mhandisi Maro alisema yanatolewa kwa mameneja ufundi na wanaohusika na usafishaji maji kwenye mamlaka hizo ili kudhibiti ubora wa maji na uwezo katika usafi wa mazingira.

"Majukumu ya mamlaka hizo za maji katika mwongozo huu, yametajwa kwenye sheria namba tano ya mwaka 2019 ya majisafi na usafi wa mazingira, ambayo ilipitishwa Julai, mwaka jana, na kuandaliwa kanuni na mamlaka ikishindwa kutimiza wajibu wake sheria itachukua mkondo wake," alisema.



Mkurugenzi wa Sekta ya Maji katika Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Mhandisi Exaud Maro (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu semina inayoendelea ya kuwajengea uwezo wa mwongozo wa namna ya uondoaji wa majitaka katika makazi kwenye maeneo yao kwa wawakilishi wa mamlaka za majisafi na taka za mikoa 26 nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Katibu Mkuu aifunda Posta utendaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano anayeshughulikia Sekta ya Mawasiliano, Dk. Zainabu Chaula, amewataka watendaji wa Shirika la Posta Tanzania kujiimarisha kiutendaji ili kushika nafasi ya kwanza barani Afrika kwa huduma bora.

Dk. Chaula aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mafunzo kwa viongozi wa shirika hilo yanayohusu uongozi na utendaji kazi, yanayofanyika jijini hapa.

Alisema kila meneja wa mkoa anatakiwa kuweka malengo ya juu ikiwamo kujitangaza zaidi kwa huduma zinazotolewa na shirika hilo.

"Shirika limepewa jukumu la kusafirisha masuala ya taasisi za umma. Kwa mfano kwa Wizara ya Afya (Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto), shirika linasafirisha sampuli za damu, sampuli za vitu vingi hadi maabara ya taifa pamoja na na mizigo. Kwa nini msitangaze kwamba posta inasafirisha mizigo ili watu waache kukimbizana na mabasi?" Alihoji.

Dk. Chaula aliwataka watendaji hao kufanya kazi kwa bidii ili kupata matokeo mazuri katika kuhudumia jamii na kupata fursa kiuchumi.

"Lazima katika kipindi cha miaka mitano ijayo tufike uchumi wa juu, lakini tutafikaje kama hatuna uwajibikaji wa pamoja wa matokeo? Tupo Tanzania ya kidigitali, tunatumia mifumo, anuani za makazi, posta kiganjani. Hakuna haja ya kukimbizana na daladala. Tuma mzigo kwa njia ya posta na utafikishiwa hadi nyumbani wakati unafanya kazi nyingine," alisema. Katibu Mkuu huyo aliitaka shirika hilo kujiimarisha zaidi kwenye utoaji huduma na kuifanya Tanzania kushika nafasi ya kwanza barani Afrika na duniani kwa utoaji huduma.

"Kila mtu akajitathmini sisi sekta ya mawasiliano ndiyo tunatakiwa kupeleka fedha mfuko mkuu wa serikali si kila siku kuomba," alisema. Awali, Mtendaji Mkuu wa Shirika hilo, Hassan Mwang'ombe, alisema mafunzo hayo yamewakusanya mameneja wa shirika hilo wa mikoa yote nchini ili kuweka mikakati juu ya kuongoza shirika kwa pamoja.

"Tunatengeneza kitu cha maelewano ya pamoja, kwani sisi ni viongozi. Kitu gani tufanye ili twende mbele, tumekusanyika hapa ili kuangalia majukumu yetu ya kila siku, kila mtu apate kupangiwa majukumu na kuyasimamia ili kupata matokeo chanya," alisema.

Mwang'ombe alisema shirika hilo linatoa huduma ya kusafirisha barua, usafirishaji wa nyaraka muhimu(EMS), uwakala ambapo kuna zaidi ya taasisi 350 ambazo zinatumia huduma ya posta huku Watanzania asilimia 50 wanatumia huduma hizo.

"Posta imejiandaa kiutendaji kazi, ndio tulikuwa wasafirishaji wakubwa wa sampuli za corona na tumefanya kwa asilimia 100, tulipeleka Dar es Salaam ndani ya saa 24," alisema.

# Mamalishe watakiwa kuzingatia usafi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MAMALISHE, kwenye masoko mbalimbali jijini Dodoma, wametakiwa kuzingatia usafi wa vifaa vyao wanavyovitumia ili kuwaepusha wateja wao na homa za matumbo.

Ofisa Masoko wa Jiji hilo, James Yuna, alitoa ushauri huo jana alipokuwa akizungumza na wajasirimali hao wanaojishughulisha na upikaji wa vyakula kwenye masoko yaliyoko jijini hapa.

Yuna aliwataka kuhakikisha maeneo hayo wanayotumia yanakuwa safi wakati wote, pamoja na wao wenyewe na vifaa vyao vinavyotumika.

Pia aliwataka kutumia fursa waliyo nayo kujiunga kwenye vikundi vitakavyowawezesha kupata mikopo mbalimbali inayotolewa na halmashauri ya jiji na taasisi za kifedha ili wainue mitaji yao.

Aliwataka pia wajasiriamali hao kufanya shughuli zao katika mtazamo utakaowafikisha kwenye malengo ya kuingia katika ushindani wa masoko.

Yuna alisema kuna baadhi ya wajasiriamali ambao ni baba na mama lishe wanafanya kazi hizo kwa mazoea bila kwenda na wakati na kushindwa kufikia malengo kutokana na maeneo yao kutoridhisha wateja wanaowahudumia.

"Dodoma ni makao makuu ya nchi na kila siku kuna makundi ya watu wanaingia hapa, hivyo niwaombe mama na babalishe ambao mmekuwa mikijishughulisha na kupika vyakula fanyeni kazi hizo kwa malengo ikiwezekana mfikie hatua ya ushindani wa masoko kupitia vyakula vyenu hivyo mnavyopika," alisema.

Katika hatua nyingine, aliwaonya wafanyabiashara wadogo kuyaheshimu maeneo ambayo yapo wazi kwa kutofanya biashara.

"Wafanyabiashara wamekuwa wakikiuka kanuni na sheria za jiji kutokana na upangaji wa biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi, suala ambalo limekuwa likihatarisha bidhaa zao na kwa wateja," alisema.





# TARI yaagizwa kufanyia utafiti masoko ya mazao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, ameiagiza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), kufanya utafiti wa masoko ya mazao ya wakulima ndani na nje ya nchi, ili kuwawezesha wananchi kuzalisha kwa tija mazao ambayo wana uhakika wa kupata soko.

Alitoa agizo hilo juzi alipokuwa anazungumza na watumishi wa TARI Kituo cha Uyole jijini Mbeya baada ya kuwatembelea wadau mbalimbali wa kilimo na kusikiliza kero zao ikiwamo tatizo la soko.

Alisema taasisi hiyo imekuwa ikifanya vizuri kwenye utafiti wa aina mbalimbali za mbegu, lakini tatizo ni kwamba baadhi ya mazao hayo yanakuwa hayazingatii mahitaji ya soko.

Naibu Waziri Mgumba alisema kwa sasa wananchi wanatakiwa kufundishwa kilimo biashara kwa kuwafundisha mbinu bora za kilimo na kuwaelekeza masoko yalipo ili wanapoanza kulima wawe wanajua watamuuzia nani.

"Ninyi watafiti ni lazima mtufanyie utafiti wa masoko yanataka nini, ubora wa bidhaa zinazohitajika, gharama za uzalishaji wa bidhaa yenyewe zikoje na zinahitajika kwa wakati gani, hapo tutakuwa tunawasaidia wakulima wetu," alisema Mgumba.

Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema maagizo hayo ya serikali wameyapokea na akaahidi kuyafanyia kazi kwa maelezo kuwa mengi yanaendana na shughuli za taasisi hiyo.

Alisema watahakikisha wanaendelea kufanya utafiti wenye tija ukiwemo wa mazao na soko la mazao hayo kama alivyoelekeza Naibu Waziri.

"Sisi tumekuwa tukifanya utafiti kwa muda mrefu na tumezalisha mbegu za mazao mbalimbali ambayo baadhi ni kwa ajili ya biashara na mengine ni kwa ajili ya lishe, kuna mbegu ambazo tumezalisha zinazaa sana zikiwamo za maharage, ulezi, mahindi, mpunga na mtama," alisema Dk. Bucheyeki.

Nao baadhi ya wadau wa kilimo ambao Naibu Waziri aliwatembelea, walisema watahakikisha wanashirikiana na Serikali kuhakikisha wakulima wanajengewa uwezo mzuri wa kuzalisha mazao yenye ubora ili kuongeza tija.

Raphael Ndelwa, ambaye ni mnunuzi wa mazao ya wakulima mkoani Mbeya, alisema wananchi wa Mkoa wa Mbeya wanafanya kazi kwa nguvu lakini tatizo ambalo huwa linawakabili ni ukosefu wa mitaji.

Alisema kutokana na tatizo hilo yeye aliamua kuanza kuwakopesha wakulima pembejeo ili wamrejeshee baada ya mavuno kwa kumpa mazao na kwamba utaratibu huo una matunda mazuri.

# Sugu ajinadi kuipaisha Mbeya Mjini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Joseph Mbilinyi 'Sugu', amewaomba wananchi wa jimbo hilo kumpigia kura Oktoba 28, mwaka huu, ili awaletee maendeleo ikiwamo kuipanua barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) kuwa ya njia nne.

Amesema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita alishindwa kutekeleza baadhi ya majukumu yake kutokana na kupitia katika kipindi kigumu ikiwamo kufungwa gerezani miezi mitano na kumpoteza mama yake ambaye anadai alifariki kutokana na kupata presha baada ya yeye (Sugu) kufungwa.

Sugu aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa kampeni uliofanyika katika Kata ya Nzovwe, ambapo alisema mbali na kufungwa, lakini chama chake pamoja na vyama vingine vya upinzani vilikuwa kifungoni kwa kuzuiwa kufanya mikutano ya hadhara.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano alifanya mikutano miwili pekee ukiwamo alioufanya kwenye uwanja wa Shule ya Msingi Mwenge ambao ndio uliomfanya afungwe jela kwa madai ya kumdhalilisha Rais John Magufuli.

Alisema lengo la serikali kumfunga ilikuwa kumdhoofisha kisiasa na kwamba kilichotokea ni kinyume chake, ambapo badala ya kudhoofika ameimarishwa zaidi kutokana na wananchi kuendelea kumkubali.

"Lengo lao ilikuwa kwamba nikitoka gerezani wananchi mtasema wanini mfungwa huyo? Na pengine walidhani nami 'ningeunga juhudi' (kuhamia CCM), lakini kinachoonekana ni kama walimpiga chura teke maana mmeonyesha imani kubwa sana kwangu," alisema Sugu.

Alisema wananchi wa Jiji la Mbeya bila kujali itikadi zao za kisiasa, walionyesha upendo mkubwa kwake alipokuwa gerezani kwa kwenda kwa wingi kumuona siku za mwisho wa wiki na kumpelekea vitu mbalimbali ambavyo alikuwa anagawana na wafungwa wenzake.

Sugu alisema pamoja na matatizo aliyopitia katika kipindi hicho, lakini alitekeleza baadhi ya ahadi zake ikiwamo ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika jiji hilo zikiwamo barabara.

Alisema wakati anaingia kwa mara ya kwanza bungeni mwaka 2010 Jiji la Mbeya lilikuwa na barabara za lami zenye urefu wa kilomita tisa pekee, lakini mpaka sasa barabara za lami zina urefu wa kilomita 70 na kwamba akichaguliwa tena atahakikisha zinajengwa zaidi.

Vilevile alisema atahakikisha mradi wa maji wa chanzo cha Mto Kiwira unakamilika kwa maelezo kuwa ndio utakuwa suluhisho la tatizo la maji katika Jiji la Mbeya na Mji wa Tunduma mkoani Songwe.

"Nimesikia kwamba kuna mtu anatembea na video alizokuwa anawaombea maji bungeni, ninyi mnakumbuka na ni mashahidi kuwa niliomba mradi wa maji wa Mto Kiwira mbele ya Rais alipokuja pale Ruandanzovwe na mradi wenyewe unagharimu Sh. bilioni 70," alisema Sugu.

Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Mbeya, John Mwambigija, 'Mzee wa upako', alisema serikali ya CCM imeshindwa kuajiri vijana katika kipindi cha miaka mitano, na kwamba hata walioajiriwa hawajapandishiwa mishahara katika kipindi hicho.

Alisema serikali imeshindwa kufufua viwanda ambavyo vilikuwa vinaajiri vijana wengi na kikiwamo cha nguo cha Mbeya, kiwanda cha majembe na kiwanda cha sabuni.

"Sasa kutokana na kukosekana kwa ajira ndiyo maana machangudoa wanaongezeka nchini ikiwamo pale Mafiati, maana hakuna ajira za kuwaingizia kipato," alidai Mwambigija.

Aliwataka wananchi kuwachagua wagombea wa CHADEMA kwa maelezo kuwa chama hicho kikishinda kitaunda serikali ambayo itakuwa rafiki kwa wananchi.



Mgombea ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Joseph Mbilinyi 'Sugu', akihutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu katika Kata ya Nzovwe, jijini Mbeya juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mikoa yaelekezwa kuandaa mipango matumizi bora ardhi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKURUGENZI Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mpango ya Matumizi ya Ardhi Tanzania, Dk. Steven Nindi, ameitaka mikoa yote nchini kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa kuhakikisha wanatenga maeneo maalum ya mifugo, ardhi oevu, hifadhi, makazi na kilimo.

Amesema lengo ni kuondokana na migogoro ya ardhi pamoja na kuhifadhi mazingira.

Dk. Nindi aliyasema hayo hivi karibuni wakati akizungumza na waandishi wa habari juu ya namna serikali inavyojitahidi katika kuhamasisha utunzaji wa mazingira na utatuzi wa migogoro inayosababishwa na ardhi. Alisema waandishi wa habari wana jukumu la kuhakikisha kupitia kalamu zao wanatoa elimu kwa wananchi umuhimu wa utunzaji mazingira sambamba na kuwakumbusha viongozi wa mikoa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za ufugaji, kilimo, hifadhi, makazi na maeneo oevu.

"Viongozi wote kuanzia ngazi ya mikoa, wilaya hadi vijiji wanapaswa kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kijamii na hii itasaidia kuepukana na migogoro ya ardhi licha ya serikali kujitahidi kutatua migogoro hiyo," alisema Dk. Nindi.

Hata hivyo alibainisha kuwa Wizara ya Kilimo na Mifugo imetenga jumla ya hekta 48,502.2 kutoka Ranchi ya Taifa na kuwapa wafugaji kwa utaratibu maalum wa muda mfupi katika maeneo ya Kongwa iliyoko Dodoma, Kalambo Katavi, West Kilimanjaro, Misenyi na Kigoma.

Na jumla ya vitalu 100 vimetengwa kati ya hivyo 93 vimekodishwa kwa wawekezaji ambao wamewekeza jumla ya ng'ombe 44,668 na kondoo 4551. Vilevile alifafanua kuwa hekta 1,3 67,994 zimetolewa na wizara kwa ajili ya malisho kutoka kwenye vituo vya kupumzisha mifugo na kati ya hizo hekta 11,598,552 katika eneo la Shoga lililopo Mbarali mkoani Mbeya zimetengwa huku hekta 7,492,00 eneo la Sangambi wilayani Chunya zimetengwa.



# Serikali yaridhishwa ujenzi barabara ya Mambosasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, imesema imeridhishwa na kiwango cha Barabara ya Mambosasa hadi Mwera iliyojengwa kwa lami na kampuni ya MECCO ya Tanzania.

Akikagua barabara hiyo jana baada ya kukamilika kazi ya kutandika lami, Waziri wa wizara hiyo, Haji Omar Kheri, alisema ni faraja kwamba ujenzi huo umemalizika kabla Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, hajamaliza muda wake wa uongozi.

Alisema, Dk. Shein ndiye aliyeagiza barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 3.4 ijengwe kwa lami ili kuwaondolea wananchi usumbufu wa usafiri.

Waziri Kheri aliipongeza MECCO kwa kuifanya kazi hiyo kwa mujibu wa kiwango kilichotarajiwa, akisema hatua hiyo inaongeza imani ya serikali kwa makandarasi wazalendo.

“Ingawa kulikuwa na changamoto ndogo zinazotuhusu sisi (serikali) na nyingine kwa mkandarasi, lakini wamejitahidi kuhakikisha wanaimaliza na kuikabidhi kwetu,” alisema.

Alihimiza kukamilishwa kwa kazi zilizobakia ikiwamo misingi ya kupitishia maji pamoja na kuwekwa alama za barabarani ili kuepusha ajali kwenye barabara zisizokuwa za lazima.

Kwa upande mwingine, alitoa wito kwa madereva wa magari ya mizigo kufuata masharti kwa kutopitisha kwenye barabara hizo yenye uzito unaozidi tani 10, na kwamba atakayeshikwa akifanya hivyo ajiandae kukabiliana na faini.

Alisema suala la kuwajengea wananchi barabara za kisasa limo katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2010-2020), ili waweze kuendesha shughuli zao za kiuchumi, biashara na kijamii na kutokomeza umaskini.

Akitoa maelezo kuhusu ujenzi huo, Injinia Mkuu wa wizara hiyo Ali Omar, alisema Sh. 3,500,000,000 zimetumika kujenga barabara hiyo na zote zimetolewa na serikali.

Alisema kazi ndogo zilizobakia zitamalizwa katika kipindi kifupi kijacho, ikiwamo kumaliza misingi na kuweka alama zinazoonyesha tani zinazopaswa kupita kwenye njia hiyo.

Kwa upande wake, Injinia wa kampuni ya ujenzi MECCO, Nassor Ramadhani Kolowa, aliishukuru serikali kupitia wizara hiyo, kwa kuwaamini kuwapa kazi akisema, hiyo ni ithibati ya kuridhika na uwezo na uzoefu walionao.

Hata hivyo, alisema katika kuhakikisha ulinzi wa barabara hiyo ambayo sasa ni tegemeo kubwa la gari za mizigo, ni jukumu la taasisi nyingine kushirikiana ili kusitokee ukiukwaji wa masharti.

Baadhi ya wananchi wa Mwera na watumiaji wengine wa barabara hiyo waliomba serikali baada ya kutandikwa lami, wizara ifikirie uwezekano wa kuweka taa za barabarani ili kulifanya eneo hilo liwe salama zaidi. Wananchi hao waliwaasa madereva wasiigeuze neema hiyo kuwa nakama kwa kuendesha mwendo kasi na kusababisha ajali hasa ikizingatiwa kuwa inatumiwa na wanafunzi wa shule iliyo karibu.



Mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, akihutubia katika mkutano wa uzinduzi wa kampeni za uchaguzi mkuu katika viwanja vya Tibirinzi, kisiwani Pemba juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mgombea ubunge afariki dunia ghafla

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Mpendae visiwani hapa kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Salim Hassan Turky, amefariki dunia ghafla usiku wa kuamkia jana visiwani Zanzibar.

Turkey alimaliza muda wake wa kulitumikia jimbo hilo kwa muda wa miaka 10 na kuomba tena ridhaa ya kuliongoza tena na CCM kumpitisha, alifariki dunia katika Hospitali ya Global iliyopo mjini hapa wakati akipatiwa matibabu baada ya kuugua ghafla.

Mtoto wa marehemu Toufiq Salum Turky, alithibitisha kifo hicho cha baba yake na maziko yake yalifanyika jana nyumbani kwake Mpendae na kwenda kuzikwa Fuoni Kijitoupele.

Septemba 12, mwaka huu, Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, alimnadi mgombea huyo Salim Turky katika uzinduzi wa kampezi za CCM zilizofanyika viwanja vya Demokrasia Kibandamaiti.

Pia Dk. Shein alimkabidhi ilani ya utekelezaji ya CCM ya mwaka 2020/2025 na Turky alijiombea kura katika uzinduzi huo wa kampeni pamoja na mgombea urais wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, mgombea urais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi na wagombea wezake kupitia CCM.

“Mimi Salim Turky mgombea ubunge wa Jimbo la Mpendae, naomba kura zenu za ndio pia nawaombea wagombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar na wagombea wote wa CCM Oktoba 28 mutupigiea kura...kinamama mtampa...mtanipa nini,” alisema Turky wakati wa uhai wake katika mkutano huo.

Wakizungumza na Nipashe wananchi wa Jimbo la Mpendae, walisema kuwa wamepata pigo kubwa kwa kuondekewa na kiongozi wao huyo ambaye walisema walijenga matumaini ya kuwaongoza tena miaka mitano ijayo.

Mashavu Shaali ni miongoni mwa wananchi hao, alisema mgombea huo wakati akiwa mbunge wa jimbo hilo alikua akiwajali wananchi wote bila ya ubaguzi wa rangi, dini, wala itikadi ya vyama vya siasa.

“Watu wa Mpendae tulikuwa na msemo wetu wa mabadiliko fasta ambao ni maarufu ulioanzishwa na Turky na kweli katika uongozi wake wa miaka 10 mabadiliko tumeyaona jimboni,” alisema.

Naye Ali Haji alieleza kuwa Tusky, aliweka mfumo maalum jimboni hapo kuwasaidia wanafunzi wasio na uwezo ambao wanataka kujiunga na elimu ya juu.

“Kwa kweli tumeondokewa wananchi wa Jimbo la Mpendae, lakini ndio kazi ya Mungu haina makosa Allah amlaze mahala pema peponi kiongozi wetu Turky,” alisema mwananchi huyo huku akimwagikwa na machozi.

Salum Turkey licha ya kuwa mwanasiasa, alikuwa mfanyabiashara maarufu visiwani Zanzibar. Alizaliwa Februari 11, 1963 na kufariki dunia Septemba 14, 2020. Mungu ailaze roho yake mahala pema peponi. Amina.

# ‘Wanawake wakipewa uongozi wanafanya vizuri’

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Kaskazini Unguja, Iddi Ame, amesema wanawake wanapopewa uongozi hufanya kazi nzuri ya kuwatumikia wananchi.

Aliyasema hayo wakati akizindua kampeni za uchaguzi za ubunge, uwakilishi na udiwani katika Jimbo la Bumbwini, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Aliwataka wananchi kuwarudisha wagombea wa CCM kushika nafasi za uongozi kwa ajili ya kuharakisha maendeleo yanapatikana na mgombea uwakilishi wa jimbo hilo ni mwanamke.

Ame alisema Jimbo la Bumbwini limepata heshima kubwa ya kuwa ndiyo nyumbani kwao mgombea wa urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM, Dk. Hussein Ali Mwinyi, hivyo haitakuwa vizuri kama jimbo hilo likachukuliwa na wapinzani.

Aliwakumbusha wananchi wa jimbo hilo kwamba katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 jimbo hilo nafasi ya ubunge lilichukuliwa na CUF kama ilivyokuwa katika uchaguzi mkuu wa kwanza mwaka 1995.

“Wananchi wa Jimbo la Bumbwini nawaomba mwaka huu turudishe heshima yetu, tumepata fahari kubwa kwamba mgombea wa urais kwa tiketi ya CCM, Dk. Hussein Mwinyi, anatoka huku nyumbani kwao...tusifanye makosa kwa sababu mwaka jana jimbo hili walilichukua wapinzani CUF,” alisema.

Naye mgombea wa nafasi ya uwakilishi jimbo hilo, Mtumwa Peya, aliwaomba wananchi na wapigakura wa jimbo hilo kumwamini na kumpa nafasi tena ya kugombea kwa kipindi kingine cha miaka mitano ili azipatie ufumbuzi changamoto zinazowakabili.

“Wananchi na wapigakura wa Jimbo la Bumbwini nawaomba mniamini tena katika kipindi cha miaka mitano kuwania nafasi ya urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi...nimejipanga kuzipatia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi,” alisema.

Mwenyekiti wa chama wa mkoa alimkabidhi ilani ya uchaguzi mgombea huyo na kutakiwa kuitekeleza na kuisimamia kikamilifu katika maeneo mbalimbali kwa maslahi ya wananchi.

“Nakukabidhi ilani ya uchaguzi ambayo unatakiwa kuitekeleza na kuisimamia kikamilifu kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa kwa maslahi ya wananchi,” alisema.

Kadhalika, mgombea ubunge katika jimbo hilo, Mbarouk Juma Khatib, aliwataka wananchi wa jimbo hilo kuacha tofauti zao na kukichagua Chama Cha Mapinduzi, kushika hatamu ya kuliongoza.

“Nawaomba wananchi mnichague ili niharakishe maendeleo katika sekta mbalimbali kwa maslahi ya wapigakura wa Jimbo la Bumbwini,” alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- Kuboresha biashara
- Kulipa kodi ya nyumba
- Kumalizia tenda
- Kulipa matibabu n.k.

Mawasiliano yetu: Dar es salaam **– 0768 928 516. Arusha – 0677 226 960.**


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**


## KUPOTEA KWA VYETI



**Patrick David Kivambe** anatangaza kupote kwa vyeti vifuatavyo; cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0140-0545** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2000 katika shule ya Sekondari Mzumbe na cheti cha kidato cha sita chenye **index namba S0140-0070** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2003 katika shule ya Sekondari Mzumbe, Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochocte cha Polisi.
Polisi Taarifa: **DAR/CHA/RB/666681/2020**

215902002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;267/2020**

**Ombi la SINA GRACEFORD CHIDUSU,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu GRACEFORD MARLEY CHIDUSU.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 07/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 11/09/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MOROGORO

115902602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;269/2020**

**Ombi la CHRISTIAN AUGUSTINO MTENGELA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu RICHARD AUGUSTINO MWELAGI.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 25/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 11/09/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU

115902802


**Uza,**

**Chenye Thamani**

**Kubwa Kwa Kutangaza**

**Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**



**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Corona yarudisha nyuma maendeleo kwa miaka 20

**WASHINGTON, Marekani**

RIPOTI ya utafiti wa wakfu wa Bill & Melinda Gates, imebainisha kuwa kusambaa kwa virusi vya corona kote duniani kumerudisha nyuma maendeleo ya dunia kwa miaka zaidi ya 20.

Kulingana na utafiti huo, mamilioni ya watu duniani wamezidi kuishi zaidi katika maisha yanayotofautiana, magonjwa na umaskini.

Wakfu huo wa Bill & Melinda Gates ulisema kuwa hali hiyo inaathiri malengo mengi ya Umoja wa Mataifa yanayolenga kuleta maendeleo duniani.

Akizungumza na BBC, Bill Gates alisema kuwa chanjo ya virusi vya corona iliyotengenezwa na kufikia kiwango stahiki huenda ikapatikana mwakani.

***BBC***



Rais mstaafu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Joseph Kabila (wa pili kushoto), amekuwa seneta wa maisha, kulingana na katiba ya nchi hiyo. **PICHA: MTANDAO**

## Kabila awasili bungeni kama seneta

**KINSHASA, CONGO**

RAIS wa zamani wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Joseph Kabila, jana aliwasili kwa mara ya kwanza katika Bunge la nchi hiyo rasmi kama Seneta.

Kwa mujibu wa katiba ya DRC kwa sababu ni Rais mstaafu moja kwa moja anakuwa seneta wa maisha.

Kabila mwenye umri wa miaka 49, alikuwa Rais wa Congo kati ya Januari 2001 hadi mwaka jana, alipoondoka madarakani baada ya uongozi wa nchi hiyo kuchukuliwa na Rais wa sasa, Felix Tshisekedi, katika uchaguzi uliotawaliwa na vurugu na maandamano.

Wengi wanamuona Kabila kama mtu mwenye ushawishi wa kisiasa katika taifa hilo na kwamba huenda akarejea tena madarakani.

Chama cha Kabila kinataka sheria ya uchaguzi nchini humo ifanyiwe mabadiliko makubwa na uchaguzi wa Rais ufanyike bungeni, badala ya Rais kuchaguliwa na wananchi.

***BBC***

## Mahakama yamzuia Ghagbo kuwania urais

**YAMOUSSOUKRO, Ivory Coast**

MAHAKAMA ya Katiba nchini Ivory Coast imemzuia Rais wa zamani wa nchi hiyo, Laurent Gbagbo na Waziri Mkuu wa zamani, Guillaume Soro, kugombea urais katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba.

Tume ya uchaguzi ilikuwa tayari imekwishasema kuwa yeyote mwenye rekodi ya uhalifu atazuiwa kugombea ambapo kwa pamoja Gbagbo na Soro walipatikana na hatia.

Awali, maandamano yaliibuka katika miji kadhaa kupinga uamuzi wa Rais Alassane Ouattara wa kugombea muhula wa tatu, kitu ambacho katiba ya nchi hiyo inazuwia.

Watu 15 walikufa katika ghasia tangu mwezi uliopita alipotangaza kwamba atagombea tena urais.

Alichukua uamuzi huo baada ya mrithi wake aliyemchagua kufa ghafla mwezi Julai.

***BBC***

## Trump kujibu shambulio la Iran mara 1,000

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ameapa kwamba shambulio lolote litakalofanywa na Iran litajibiwa mara 1,000 kwa ukubwa, baada ya ripoti kuwa nchi hiyo inapanga kulipiza kisasi baada ya kuuliwa jenerali wa ngazi ya juu Qasem Soleimani.

Ripoti ya vyombo vya habari nchini Marekani, zimenukuu maofisa ambao hawakutajwa majina, wakisema kuwa mpango unaodaiwa kupangwa na Iran wa kumuua balozi wa Marekani nchini Afrika Kusini ulipangwa kabla ya uchaguzi wa rais mwezi Novemba.



Kwa mujibu wa ripoti za vyombo vya habari, Iran inaweza kuwa inapanga mauaji hayo, ama mashambulizi mengine, dhidi ya Marekani kwa kulipiza kisasi kwa kuuliwa kwa Jenerali wa Iran Soleimani, Trump aliandika katika ukurasa wa Twitter.

Alisema shambulio lolote litakalofanywa na Iran, kwa njia yoyote ile, dhidi ya Marekani litajibiwa kwa shambulio kubwa zaidi ambalo litakuwa mara 1,000 zaidi kwa ukubwa.

**DW**

## Museveni aadhimisha miaka 76 ya kuzaliwa

**KAMPALA, Uganda**

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, jana aliadhimisha siku yake ya kuzaliwa akitimiza umri wa miaka 76.

Museveni ni miongoni mwa marais wa Afrika waliohudumu kwa miaka 34 kwenye nafasi hiyo baada ya kuiingia mwaka 1986.

Rais huyo ametangaza nia yake ya kuwania kiti hicho cha urais baada ya kuidhinishwa na chama chake cha NRM kupeperusha bendera katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwakani.

Mtoto wa Rais Museveni, Muhoozi Kainerugaba alikuwa ni miongoni mwa raia wa Uganda walituma ujumbe wa kumtakia kila la heri katika siku ya kuzaliwa kupitia mitandao ya kijamii.

"Heri ya siku ya kuzaliwa mzee wa kazi na Baba wa Taifa. Mwenyezi Mungu aendelee kukubariki," aliandika Kainerugaba.

**BBC**

## Guterres kuyataka mataifa kusitisha mapigano

**NEW YORK, Marekani**

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, anatarajia kutumia hotuba yake ya kila mwaka kwa viongozi wa dunia wiki ijayo kusukuma ajenda ya kusitisha mapigano duniani hadi mwishoni mwa mwaka huu, ili nchi ziweze kupambana na janga la virusi vya corona.

Guterres alisema fursa zitakuwa zimepotea kwa sababu viongozi wa mataifa hawatakuwapo binafsi mjini New York kwa ajili ya mkutano huo.

Guterres alisema usitishaji wa mapigano duniani utaimarisha juhudi za kupambana na corona na kusaidia kurejea katika hali ya kawaida kwa njia iliyoratibiwa vizuri na endelevu.

Hapo awali alitoa wito wa kusitishwa mapigano Machi 23, mwaka huu, lakini uungwaji mkono rasmi kutoka kwa wanachama 15 wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ulichukua zaidi ya miezi mitatu, kwa sababu ya mkwamo kati ya China na Marekani.

Marekani haikutaka azimio hilo lizungumzie kuhusu Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), wakati China ilitaka hivyo.

**DW**



# CAVANI
## AWANIWA NA GREMIO YA BRAZIL

**RIO DE JAINERO, Brazil**

RAIS wa klabu ya Gremio, Romildo Bolzan Junior, ana matumaini ya kufanya mazungumzo na Edinson Cavani, juu ya kuhamia katika klabu hiyo ya Brazil.

Cavani kwa sasa ni mchezaji huru, akiwa ameondoka kule Paris Saint-Germain baada ya mkataba wake kumalizia Juni, akiwa amekaa misimu saba kule Paris.

Cavani ambaye ameweka rekodi ya ufungaji wa wakati wote kule Paris, akiwa na mabao 200 aliyofunga katika mashindano yote, amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa kubwa za Ulaya ikiwamo Inter Milan, Bayern Munich na hivi karibuni Barcelona.

Pia, ilibainishwa kwamba, nyota huyo mwenye umri wa miaka 33 anaweza kuchagua kurudi barani Amerika Kusini, huku Gremio ndio klabu inayotajwa kumwania.

Makamu wa Rais, Paulo Luz alikanumadai ya kuzungumza na mwakilishi wa Cavani, lakini Romildo bado hayupo tayari kuondoa uwezekano huo kwa kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa Uruguay.

"Yeye (wakala wa Cavani) hajapata ofa yoyote. Lakini katika maisha kama huongei huwezi kujua chochote," alisema akiiambia Hora do Consular.

"Kwa sasa siwezi kusema kwamba hakuna uwezekano wa kuzungumza naye, kwa sababu lolote kwa wakati wowote linaweza kutokea."

Cavani alishinda mataji 19, yakiwamo sita ya Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, baada ya kujiunga na PSG akitokea Napoli mwaka 2013 kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 64.

## Depay kujiunga Barcelona wiki hii

**BARCELONA, Hispania**

NYOTA wa Lyon, Memphis Depay atajiunga na Barcelona kwa ada inayotajwa kuwa euro milioni 30 wiki hii, kwa mujibu wa gazeti la De Telegraaf.

Barcelona wanaonekana kuwa kwenye nafasi kubwa zaidi ya kumsajili Depay, baada ya kuonekana kushindwa kumshawishi, Lautaro Martinez kuondoka kule Inter Milan.

Baada ya kumaliza msimu wa 2019-20 bila taji lolote, miamba hao wa LaLiga, Barca kwa sasa wanajijenga upya chini ya kocha mpya, Ronald Koeman.

Nyota kadhaa wametajwa kuwaniwa na Barca, lakini Depay ndio kwa sasa anaonekana kuwa njiani kuelekea kule Camp Nou.

Kwa mujibu wa ripoti kutoka nchini Hispania, Barcelona watakamilisha usajili wa nyota huyo wiki hii.

Kama uhamisho huo utafanikiwa, Depay atajiunga na kocha wake wa zamani wa timu ya taifa ya Uholanzi, Koeman.

Depay alifunga mabao 15 katika mechi 22 kwa Lyon msimu uliopita.

# Lampard: Werner atakuwa fiti kuivaa Liverpool

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard ana matumaini Timo Werner atakuwa fiti kuivaa Liverpool baada ya kuumia mguu, huku Christian Pulisic akiwa amepona.

Werner alishinda penalti katika mchezo wake wa kwanza kwa Chelsea, wakati kikosi hicho cha Lampard kikiibuka na ushindi wa 3-1 dhidi ya Brighton and Hove Albion kwenye Ligi Kuu England, juzi Jumatatu.

Wakati fowadi huyo alicheza kwa dakika 90, Lampard alithibitisha Werner aliumia mguu, ingawa anamtarajia mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani kuwa tayari kuivaa Liverpool kule Stamford Bridge, Jumapili.

"Timo aliumia wakati akishinda penalti," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Matumaini yangu atakuwa fiti kwa ajili ya kuivaa Liverpool, bila shaka yoyote anaweza kucheza wiki ijayo."

Chelsea katika mchezo wao wa ufunguzi wa ligi hiyo, walikuwa bila Pulisic ambaye alikuwa anasumbuliwa na maumivu ya nyama za paja, aliyoyapata wakati wa fainali ya Kombe la FA, ambapo walifungwa na Arsenal, Agosti Mosi.

Lampard alithibitisha kwamba, mchezaji huyo wa kimataifa wa Marekani sasa amerudi na alikuwa tayari kucheza dhidi ya Brighton na atacheza dhidi ya Liverpool.

## HABARI MICHEZO



# BABA
## YAKE ALABA AMJIA JUU HOENESS

**MUNICH, Ujerumani**

BABA mzazi wa David Alaba, amemshutumu Uli Hoeness kwa "kumchafua kwa uwongo" mlinzi huyo wakati huu wakiwa kwenye mjadala wa makubaliano ya kusaini mkataba mpya na Bayern Munich.

Rais wa zamani wa Bayern, Hoeness alisema wiki hii kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 hatakiwi kuendeshwa na fedha ili asaini mkataba mpya, huku wa sasa ukiwa unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2020-21.

Nyota huyo wa kimataifa wa Austria, Alaba alijiunga na akademi ya Bayern mwaka 2008 na ameshinda mataji tisa ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, na sasa ameripotiwa kuwaniwa na timu kama Manchester City na Barcelona.

Baba yake George, amemshutumu kwa hasira Hoeness kwa kauli yake kwamba mwanawe anataka fedha nyingi, akibainisha kwamba aliacha nafasi nyingi za kuondoka kwenye klabu hiyo hapo kabla.

"Nilimpeleka David Alaba pale Bayern akiwa kijana mdogo," alisema akiiambia Sky Sport.

"Kwa miaka mingi, kulikuwa na nafasi kadhaa za yeye kuondoka na kwenda klabu nyingine, lakini tulikuwa watiifu kwa klabu na alichagua kubakia.

"Sikutarajia Bayern wangeeneza habari chafu za uwongo kuhusu Alaba, kwani amekuwa mtiifu mno kwao."



## TONALI: NILICHAGUA KUJIUNGA NA MILAN

**MILAN, Italia**

SANDRO Tonali amesema "alifunga milango mingine" wakati klabu yake ya utotoni, AC Milan ilipoweka wazi inataka kumsajili.

Wiki iliyopita Milan ilitangaza kumsajili nyota huyo wa kimataifa wa Italia kwa mkopo, huku kukiwa na kipengele cha kumsajili kwa euro milioni 35 baada ya kutamba kwa misimu mitatu akiwa na Brescia.

Tonali, ambaye analinganishwa na gwiji wa Italia, Andrea Pirlo, awali alionekana kuwaniwa na wapinzani wao Inter Milan, lakini amesema nafasi ya kujiunga na Rossoneri lilikuwa jambo zuri zaidi.

"Tangu nikiwa mtoto naishabikia Milan na baba yangu ndiye aliyenirithisha ushabiki huu," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilitaka kuvaa jezi nyeupe. Sikuzungumza sana na Massimo Cellino (rais wa Brescia), lakini alijua nini kilichopo kwenye akili yangu. Aliniambia nifanye mwenyewe maamuzi.

"Nilimwambia wapi ninakotaka kwenda na nilimuomba anisaidie na haraka ikatokea nafasi kule Milan, na nikaamua kufunga milango yote. Nikaamua kwenda Milan.

"Na kwa sasa nipo katika klabu ya ndoto zangu na nina furaha kubwa kuwa hapa nasubiria kwa hamu kubwa kuichezea klabu hii."

# Sancho haondoki Dortmund, asema kocha

**DORTMUND, Ujerumani**

KOCHA Lucien Favre amebainisha kwamba, fowadi Jadon Sancho hataondoka Borussia Dortmund licha ya kuwa na taarifa kwamba anawaniwa kwa udi na uvumba na Manchester United.

Sancho amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia United kwa kipindi chote cha dirisha hili la usajili baada ya kuwa na msimu wa kuvutia kule Dortmund.

Mkurugenzi wa Michezo wa Dortmund, Michael Zorc aliwataarifu miamba hao wa Ligi Kuu ya England mwezi uliopita kwamba hawana nafasi ya kumsajili straika huyo baada ya muda waliouweka wa Agosti 10 kupita.

United imeripotiwa bado inajaribu kutaka kumshawiki mchezaji huyo na klabu yake, lakini Favre amebainisha wazi kwamba, Sancho ni sehemu muhimu ya mipango yake kwa ajili ya msimu huu mpya.

"Tunamhitaji. Kila mmoja ana furaha kwa sababu anabaki," alisema Favre akiiambia Keystone-SDA.

"Hatuhitaji kuzungumza kuhusu ubora wake kwani ana kila kitu na wengi wanalijua hilo. "Anafunga na kutengeneza mabao na mara kwa mara anatengeneza tofauti, lakini kuna sehemu Sancho anahitaji kuimarika zaidi. Na hilo ni jambo la kawaida kwa mchezaji mwenye umri wa miaka 20."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LIONEL MESSI MWANASOKA ANAYELIPWA ZAIDI DUNIANI

Ronaldo amfukuzia nafasi ya pili huku Neymar, Mbappe na Pogba watinga 10 bora kwa mkwanja mrefu...

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi amerudi katika nafasi ya kwanza kwa mujibu wa jarida la Forbes, kuwa mwanasoka anayelipwa zaidi duniani baada ya kuingiza kiasi cha dola milioni 126, kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita, huku Cristiano Ronaldo akimkaribia nafasi ya pili.

Nyota huyo wa Barcelona aliutikisa ulimwengu wa soka mwezi uliopita, wakati alipoiambia klabu hiyo aliyokaa nao karibia kipindi chote cha maisha yake ya soka kwamba anataka kuondoka baada ya kumaliza msimu 2019-20 bila taji lolote.

Messi aliamini anaweza kutumia kipengele cha mkataba wake kuondoka akiwa mchezaji huru, lakini Barca na LaLiga walizuia hilo na kumtaka kuondoka kwa kulipa kiasi cha euro milioni 700.

Baada ya vuta ni kuvute na bodi ya klabu hiyo pale Camp Nou, Messi aliamua kubadilisha uamuzi na kutangaza kubakia kwa miamba hao wa LaLiga kwa msimu wa 2020-21.

Na sasa ametangazwa kuwa ndiye mchezaji anayelipwa kiasi kikubwa zaidi cha fedha duniani, baada ya kuingiza dola milioni 126 kwa mshahara na bonasi kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita. Mpinzani wake wa muda mrefu, Ronaldo anashika nafasi ya pili katika orodha hiyo baada ya kuingiza kiasi cha dola milioni 117.

Nyota wa Paris Saint-Germain, Neymar (Dola Mil 96) na Kylian Mbappe (Dola Mil 42) wanashika nafasi ya tatu na nne, huku fowadi wa Liverpool, Mohamed Salah akiwa nafasi ya tano akiwa anaingia dola milioni 37.

Katika kukamilisha 10 bora, wapo washindi wa Kombe la Dunia, Paul Pogba (Dola Milioni na Antoine Griezmann (Dola Milioni 14), nyota wa Real Madrid, Gareth Bale (Dola Mil 29, straika wa Bayern Munich, Robert Lewandowski (Dola Mil 28 na golikipa wa Manchester United, David De Gea (Dola Mil 27.

## KWA UFUPI

**LIVERPOOL NJIA YEUPE ALCANTARA**

KLABU ya Liverpool itasubiri hadi wiki ya mwisho ya dirisha la usajili, ili kumsajili rasmi kiungo wa kati wa Bayern Munich, Thiago Alcantara mwenye umri wa miaka 29. ***(Talksport)***

**MAN KUMCHUKUA KWA MKOPO BALE**

MANCHESTER United ipo tayari kumchukua winga wa Real Madrid, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 31 kwa mkopo, kwa makubaliano ya kumpa mkataba wa kudumu baada ya kuonekana kumkosa winga wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho menye miaka 20. ***(Sun)***

**MAN UNITED WAHOFIA USHINDANI KWA SANCHO**

MANCHESTER United inahofia kuongezeka kwa ushindani katika mbio za kumnasa Jadon Sancho msimu ujao, ikiwa hawatamchukua katika msimu huu wa dirisha la usajili. ***(ESPN)***

**MESSI KUKATWA MSHAHARA**

NYOTA wa Barcelona, Lionel Messi, ataombwa na rais wa klabu hiyo, Josep Maria Bartomeu kukatwa mshahara. ***(Deportes Cuatro)***

**ORIGI SASA AGOMBEWA**

KLABU ya Fenerbahce iko kwenye mazungumzo na Liverpool kuhusu kumsajili mshambuliaji, Divock Origi, huku Aston Villa, Newcastle, Brighton na Fullham zikimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Mirror)***

**ARSENAL KUMRUHUSU TORREIRA**

ARSENAL inaweza kumruhusu Lucas Torreira mwenye umri wa miaka 24, kuondoka kwa mkopo kabla ya msimu wa dirisha la usajili kumalizika, huku Fiorentina na Torino wakiwa wanamtaka kiungo huyo wa kati. ***(Guardian)***

**KOULIBALY AWEKEWA HATIMA**

KAMA Manchester City au Paris St-Germain hawatamaliza mchakato wa kumnyakua Kalidou Koulibaly hadi mwishoni mwa wiki hii, Napoli wanatarajiwa kumtoa sokoni mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Football)***

**MAN WATETA KUHUSU REGUILON**

MANCHESTER United wako kwenye mazungumzo na Real Madrid kwa ajili ya kumsajili, Sergio Reguilon raia wa Hispania. ***(Marca)***

**SEVILLA YAMSAJILI MARCOS**

KLABU ya Sevilla, ambayo Sergio Reguilon ameichezea kwa msimu uliopita kwa mkopo, imemsajili mlinzi wa kushoto wa Sporting, Marcos Acuna mwenye umri wa miaka 28. ***(Evening Standard)***

**WEST HAM YAKOMAA NA TARKOWSKI**

KLABU ya West Ham wanajaribu kumnasa mlinzi wa Uingereza, James Tarkowski mwenye umri wa miaka 27, baada ya Burnley kukataa ofa ya awali ya pauni milioni 30. ***(Evening Standard)***

**SUAREZ KUMALIZIA MKATABA BENCHI**

NYOTA wa Barcelona, Luis Suarez anatarajiwa kumaliza msimu wake akiwa benchi, wakati mkataba wake ukikaribia kumalizika. Suarez mwenye miaka 33 raia wa Uruguay, ameambiwa atafute klabu mpya huku akiwa amebakiza mwaka mmoja katika mkataba wake. ***(ESPN)***



HABARI MICHEZO

# PEMBA KUINUA UTALII AKIMUUNGA MKONO JPM

**Na Mwandishi Wetu**

KUFUATIA juhudi mbalimbali za maendeleo zinazofanywa na Rais Dk. John Magufuli, promota wa michezo na mitindo Mtanzania anayeishi Uganda, Jackson Pemba, amesema anatarajia kurejea nchini kuwekeza katika sekta ya utalii.

Pemba aliliambia gazeti hili kuwa, Rais Magufuli ameimarisha amani na umoja wa kitaifa, hivyo anajiandaa kuleta wawekezaji kwenye sekta ya utalii na atasaidia kuwashawishi wawekezaji wengine kuwekeza katika biashara ya hoteli, ambayo itasaidia kuinua pato la nchi.

"Niko karibu sana na mmiliki wa hoteli maarufu duniani za Marriots, tayari nina mialiko ya serikali za nchi za Malawi na Botswana, ili nao waangalie fursa na uwekezaji wa nchi hizo nilizozitaja awali," alisema Pemba.

Aliongeza anapenda kuona kazi zake zinafanyika kwa kiwango cha juu, zilizofanyiwa utafiti kila wakati na kukuza dhana za biashara, ambazo zingevutia masoko yake lengwa kufungua njia mpya na pia kurudisha kwa jamii.

Alisema, katika mipango yake ya kukuza michezo nchini, ameanzisha kampuni iitwayo Pemba Sports Africa na tayari imeshafanya kazi mbalimbali Uganda.

"Mimi ni wakala wa michezo mwenye uzoefu wa zaidi ya miaka 15, hamu yangu ni kuendeleza urithi wa michezo wa baba yangu (Cuthbert Pemba), ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa Klabu ya Michezo ya Simba ya Dar es Salaam, Tanzania," alisema Pemba ambaye aliwahi kufanya majaribio kwenye akademi ya Carlyle United na New Castle United zote za England.

Alieleza anatarajia pia, kutumia urafiki wake na wachezaji wakongwe wa England, kama Alan Shearer, Luis Ferdinand, Kevin Keegan, Warren Burton, Robert Lee, John Barnes na Stuart John Hall, ili kukuza michezo ya ndani.

Mbali na kuweka nguvu kwenye soka, pia anamiliki timu ya mpira wa kikapu ya Pemba Warriors, huku kituo chake kikishiriki katika mashindano ya magari ya Omutima na vile vile anasimamia timu ya soka ya taasisi ya Selimundu.

"Lengo letu ni kubadilisha na kuwezesha tasnia ya michezo nchini Tanzania, kwa kutoa huduma muhimu za kimkakati kwa klabu za michezo kitaalamu, mashirikisho ya kitaifa, watu binafsi na kampuni zinazovutiwa na michezo," alisema Pemba.

Mfanyabiashara huyo pia ni rais wa WFM, kampuni ya kimataifa ambayo huwatafutia mapambano ya kimataifa mabondia wa kickboxing duniani.



Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia (kushoto) na Rais wa Shirikisho la Soka Burundi (BFF), Reverien Ndikuriyo, wakizindua semina ya utawala ya viongozi wa soka wanawake itakayofanyika kwa muda wa siku tano hapa jijini, Dar es Salaam. Kozi kama hiyo pia itaendeshwa katika mikoa mingine tisa hapa nchini. **PICHA : SOMOE NG'ITU**

# KMC yaendelea kung'ara Bara

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21, imekuwa njema kwa timu ya KMC ya Kinondoni kwenye mechi mbili za kwanza, baada ya kuongoza kwa muda wa wiki mbili mfululizo.

Hii ni kwa mara ya kwanza tangu kupanda daraja na kuanza kucheza Ligi Kuu msimu wa 2018/19.

KMC ambayo msimu uliomalizika haikuwa kwenye hali nzuri na ilibidi isubiri mechi za mwisho ibakie Ligi Kuu, ilianza kuongoza msimu huu baada ya kuitwanga Mbeya City, mabao 4-0 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini, Dar es Salaam.

Hakuna timu nyingine baada ya raundi ya kwanza kumalizika, iliyoweza kushinda idadi hiyo ya magoli, hivyo kuifanya timu hiyo kuongoza ligi kwenye wiki ya kwanza.

Mechi ya raundi ya pili, KMC iliichapa Prisons mabao 2-1, hivyo kuzoa pointi sita, lakini ikiongoza kwa kuwa na mabao sita ambayo ni mengi zaidi kuliko timu nyingine yoyote kwenye ligi hiyo.

Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Habib Kondo, amesema kuwa baada ya kucheza kwa msimu miwili Ligi Kuu, msimu huu wa tatu wameshakuwa wazoefu, hivyo sasa wanachohitaji ni kugombea ubingwa.

"Msimu wa kwanza ulikuwa mzuri sana mpaka tukacheza michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika. Wa pili haukuwa mzuri na tuliponea chupuchupu kushuka, lakini huu wa tatu tumeona yaliyotokea na tayari tumeshakomaa, hivyo msimu huu sasa lengo letu ni kushindana kuwania ubingwa wa Tanzania Bara," alisema Kondo.

KMC sasa inajiandaa kuelekea Shinyanga, kuwafuata Mwadui FC katika mechi ya raundi ya tatu itakayochezwa Septemba 21, mwaka huu mkoani humo.

## KMKM yawanasa wachezaji wanne

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

ILI kuongeza nguvu katika kikosi chake kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar, uongozi wa KMKM umetangaza kuwasajili wachezaji wapya wanne, imeelezwa.

Ligi Kuu Zanzibar msimu wa 2020/ 21 umepangwa kufanyika kuanzia Novemba 7, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema timu hiyo imesajili wachezaji wenye kukabiliana na ushindani uliopo kwenye ligi kwa lengo la kuhakikisha wanafanya vizuri zaidi ya msimu uliopita.

Msimu aliwataja nyota hao waliowasajili ni pamoja na mabeki, Ibrahim Hamad "Baka", Ali Juma Marifa "Mabata" wote kutoka Malindi, kiungo Greyson Gwalala "Dante" (Mlandege) na Ahmed Is-hak Haji "Beto" kutoka Jang'ombe Boys.

"Tumefanya usajili wa wachezaji kulingana na mapungufu yaliyojitokeza katika msimu uliopita ikiwamo safu ya washambuliaji, walinzi na hata mabeki wa kati, tunaamini makosa tuliyokuwa nayo hayatarejea tena," alisema kocha huyo.

Aliongeza, kikosi chake kitaanza mapema maandalizi kwa sababu wanaamini kila timu inajiimarisha kwa ajili ya kupambana kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar na kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa.

Aliwataka mashabiki wa KMKM kuendelea kuisapoti timu hiyo kwa kuhudhuria kwa wingi katika mechi zake, ili kuongeza hamasa ya kujituma kwa wachezaji wao na hatimaye malengo waliyonayo yatimie.

## Kondo afunguka kilichoibeba KMC

**Na Adam Nyangasa, TUDARCo**

KOCHA mkuu wa KMC FC, Habibu Kondo, amesema matokeo mazuri ya timu yake yametokana na maandalizi waliyofanya na hawataki kuona wanakaa 'mkiani' kama ilivyokuwa katika msimu uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kondo aliliambia gazeti hili malengo yake msimu huu ni kupata alama muhimu katika kila mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwamo dhidi ya Mwadui FC, itakayochezwa Septemba 21, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kambarage, Shinyanga.

Kocha huyo alisema kikosi chake kipo 'fiti', kuendelea kupambana na kwao kila mechi ni muhimu kwa ajili ya kuelekea kwenye mbio za ubingwa.

Alisema wanaendelea na mazoezi na kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza kwenye mechi mbili za mwanzo licha ya kupata ushindi wa asilimia 100.

"Tumepata ushindi mechi mbili za kwanza, ila ushindi huo hatuwezi kubweteka na kuhakikisha wachezaji wangu wataendelea kupambana kutafuta alama tatu kwa kila tutakayekutana naye," alisema Kondo.

Aliongeza mipango waliyonayo ni kupata matokeo chanya watakapocheza nyumbani na ugenini kwa sababu kwenye mpira lolote linaweza kutokea.

"Tunahitaji kutumia vizuri hizi mechi za kwanza kupata matokeo, hatutaki kuona makosa ya nyuma yakirudia kwa kumaliza msimu kwa presha kubwa," alisema Kondo. KMC ndio vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, wakiwa na pointi sita baada ya kupata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Mbeya City na mchezo uliopita waliwafunga Tanzania Prisons magoli 2-1.

# Michezo

Jumatano Septemba 16, 2020

Nipashe



MESSI MWANASOKA ANAYELIPWA ZAIDI DUNIANI HABARI UK 22

## SIMBA, BIASHARA HESABU ZITAONGEA

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Simba kikianza mazoezi kuikabili Biashara United, kila upande unatabiri mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Taifa jijini, Dar es Salaam utakuwa wenye ushindani.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, aliliambia gazeti hili kikosi chake kimeanza kujiimarisha kuelekea mchezo huo na lengo ni kurekebisha makosa yaliyotokea katika mechi iliyopita.

"Mpira ni mchezo wa makosa, tumeshafunga hesabu za mechi iliyopita, sasa tunajiandaa kuikabili Biashara, akili zetu ni kuona tunapambana kusaka ushindi," alisema Rweyemamu.

Naye Kocha Mkuu wa Biashara United, Francis Baraza, alisema mechi dhidi ya Simba itakuwa ngumu kwa sababu wanacheza na timu yenye kibarua kimoja cha kutetea ubingwa wanaoushikilia.

Baraza alisema wataingia uwanjani kwa kuwaheshimu, lakini wakiwa na lengo la kutafuta alama muhimu katika mchezo huo wa raundi ya tatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha huyo alisema licha ya kupata ushindi katika michezo yao miwili iliyopita, hawatabweteka na ataendelea kupanga mbinu zaidi za ushindi dhidi ya vigogo hao wa soka nchini.

Alieleza maandalizi ya mechi hiyo yatakuwa tofauti na jinsi alivyocheza mechi zao mbili zilizopita dhidi ya Gwambina na Mwadui FC, kwa sababu ya aina ya wachezaji wanaotarajia kukutana nao.

"Mechi hiyo ni ngumu, hatuwaogopi ila ninawaheshimu. Watu wanatakiwa watambue tunaenda kucheza na mabingwa, lazima uwape heshima yao, ukizingatia ni timu nzuri yenye wachezaji wazuri ambao wanaweza kumpa kocha matokeo wakati wowote wanapoamua kucheza," Baraza alisema.



Mchezaji mpya wa Chelsea, Timo Werner (kushoto), akielekea kudondoka baada ya kufanyiwa madhambi na golikipa wa Brighton, Mat Ryan (kulia), katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi usiku. Chelsea ilishinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**

# ZLATKO: GARI LIMEWAKA YANGA

### ●●●Kikosi chake kitaanza safari ya kuelekea Bukoba kesho, huku akitamba kucheza soka la...

**Na Saada Akida**

USHINDI ndio jambo pekee ambalo Kocha Mkuu wa Yanga, Mserbia Zlatko Krmpotic, analifikiria kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar utakaochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Kaitaba ulioko Bukoba, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zlatko alisema kikosi chake kipo tayari kwenda kupambana katika mchezo huo na mingine ya ugenini kwa sababu wanahitaji kupata pointi tatu kwenye kila mechi.

Zlatko alisema licha ya kupata ushindi katika mechi iliyopita, anayafanyia kazi mapungufu ya kikosi chake na anaimani ya kufanya vizuri katika michezo yao ijayo ikiwamo dhidi ya Kagera Sugar.

Kocha huyo alisema anahitaji timu yake kucheza soka la kiwango cha juu na ili kufikia huko, kila mchezaji anatakiwa kuonyesha uwezo wake halisi baada ya kukamilisha programu maalumu za mazoezi alizotoa.

Alisema kwa muda mfupi alikuwa nao amebaini wachezaji wake wanahitaji mazoezi kujijenga ambayo yatawaimarisha na kuwasaidia kuingia kwa haraka katika mfumo wake ambao utawafanya wapate matokeo mazuri katika mechi zinazofuata.

"Bado timu haijacheza vile ninavyotaka, ila wachezaji wangu wanapambana na kujitoa, nina imani kila siku zinavyozidi kwenda, kikosi kitakuwa imara, sasa akili yetu inajiandaa na mechi ijayo, tutahakikisha pia tunapata alama zote tatu muhimu katika mchezo huo," alisema Zlatko.

Alisema tayari ameshawafahamu wapinzani wao Kagera Sugar baada ya kupata taarifa zao kutoka kwa wasaidizi wake ambao wamekuwa karibu wakisaidia kutelekeza majukumu yake vizuri.

"Nimepata taarifa zote kuhusu Kagera Sugar, kupitia taarifa hiyo, nimeshaandaa mbinu na mifumo tofauti ambayo inaweza kutumia kwenye mechi hiyo, nimewajua na tutajipanga kuwakabili," Zlatko alisema.

Naye meneja wa timu hiyo, Hafidh Saleh, alisema katika kukijenga vema kikosi chao kuelekea mchezo huo wa kwanza wa ugenini, leo usiku kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini, Dar es Salaam, walitarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Mlandege kutoka Zanzibar.

"Tutacheza mechi ya kirafiki dhidi ya Mlandege, hii itampa mwanga wa kuona maelekezo yake aliyowapa wachezaji mazoezini walivyoyafanyia kazi, itamsaidia kiufundi kubaini mahali walipoimarika na idara inayohitaji kuboreshwa," alisema meneja huyo.

Alisema wanatarajia kuondoka jijini kesho na kuelekea Bukoba huku wachezaji wao wakiwa 'fiti' kwenda kupambana kusaka ushindi dhidi ya Kagera Sugar ambayo pia imekuwa ikiwasumbua kila wanapokutana.

Yanga inakutana na Kagera Sugar ambao wametoka kulazimisha sare ya bila kufungana na Gwambina FC kwenye Uwanja wa Gwambina Complex wakati wao wanakumbukumbu ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mbeya City.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >